

**SIMBA YAHITAJI 9 KUFUNGA MWAKA**

UKURASA 24

**TUHUMA ZA BIL 8.9/-** Kesi ya watumishi Dar mbioni kutua Mahakama Kuu

UKURASA 3

**TRC** yatangaza safari za treni mikoa kaskazini

UKURASA 7



**VURUGU**, dosari uchaguzi DRC, waangalizi rasmi waanika kasoro

UKURASA 19


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ijumaa Desemba 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581532

www.ippmedia.com

E & FOLLOW US twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


## SHERIA UCHAGUZI

# Vyama vyaja juu miswada yake imejaa matobo



**CCM** yaomba utulivu, yanajadilika... *Endelea ukurasa 2*



## Makonda: Sijakanyaga Kigamboni tangu nipigwe chini mwaka 2020

UKURASA 2




UKURASA WA 24

## YANGA: TABORA UNITED JIPANGENI

WAKATI timu bado ikiwa na joto la ushindi wa mechi ya mashindano ya kimataifa, benchi la ufundi la Yanga limesema watatumia nguvu ile ile kuikabili Tabora United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ulioko...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa nne kulia) na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Ali Ameir, wakifungua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa maegesho ya magari Malindi, Wilaya ya Mjini jana katika shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## Ikibaki wiki; 84% viongozi hawajaanika utajiri wao

UKURASA 4

**MICHEZO** TWENDE ZETU IVORY COAST KI-VIP, WASHINDI WAZAWADIWA UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Makonda: Sijakanyaga Kigamboni tangu nipigwe chini mwaka 2020

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amesema tangu alipoanguka katika kinyang'anyiro cha ubunge mwaka 2020, hajawahi kukanyaga Kigamboni, akiwataka wanaosaka ubunge na udiwani kwa sasa kuacha mchezo huo.

Julai 20, 2020, Makonda ashindwa katika uchaguzi wa ndani ya chama wa kumpata Mgombea Ubunge wa Jimbo la Kigamboni kupitia CCM, akipata kura 122 dhidi ya 190 za Faustine Ndugulile.

Makonda alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwapo baadhi ya makada walioanza kufanya alichokiita chokochoko za kuutaka ubunge na udiwani wakati muda wa mchakato huo haujafika.

Alisema ni vizuri viongozi waliopo madarakani wakaachwa kusumbuliwa ili watekeleze kazi zao huku akijitolea mfano yeye kwamba hajawahi kukanyaga Kigamboni, lengo likiwa ni kutoa nafasi kwa aliyeshinda kutekeleza majukumu yake.

"Chama kinatoa rai, wapo watu tunakwenda mwaka 2024 na 2025 wana shauku ya kutaka majimbo, wana shauku ya kutaka udiwani. Chama kinasema bado tuna madiwani wa CCM na wabunge.

"Maelekezo ya chama; chokochoko zote zinazofanywa ziachwe, tuwape nafasi wabunge wafanye kazi zao na katika hili huwa ninapenda kutoa mfano mimi niligombea Kigamboni mwaka 2020 nikashindwa kwenye kura za maoni, akateuliwa mgombea wa chama, akapeperusha bendera na akanadi ilani ya CCM. Mpaka leo (jana) hii tunavyoongea, sijawahi kukanyaga Kigamboni," alisema.

Makonda alisema amemwacha mbunge wa CCM kufanya kazi yake, hivyo kama kuna mtu alishawahi kugombea au ana ndoto ya udiwani ama ubunge, chama kinawatambua wabunge waliopo ni viongozi halali, wawape nafasi ya kutimiza majukumu yao.

"Habari ya kupitapita, harambee, michango mara maneno, wewe ndio mwenyewe tunakutegemea mara kundi hili tumekuanzishia la WhatsApp, tunawanyima utulivu wabunge wetu kufanya shughuli zao za kibunge. "Wakati utakapofika chama kitatoa utaratibu na kuingia katika mchakato. Kama unataka jimbo, utajionesha ila kwa sasa tungetamani kuheshimu taratibu zetu za kichama, tuwaheshimu viongozi wetu walioshinda na kupewa ridhaa ya kuongoza na tuwape ushirikiano," alisema Makonda.

Alisema kumyumbisha diwani au mbunge ni kukwamisha utekelezaji wa ilani ya CCM, hivyo viongozi waliopo wasisumbuliwe, wenye nia wasubiri taratibu rasmi zitakazotangazwa na chama.

Katika hatua nyingine, Makonda alisema CCM imewataka watendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO) kujitathmini kama wanaendana na kasi ya Rais Samia kutokana na mgawo wa umeme kuendelea kutikisa nchini, akisisitiza kuwa baadhi yao ni wazembe.

"Chama kinataka kupeleka salamu kwa TANESCO, je, maumivu, mzigo, uchungu na shauku anayoibeba Rais Samia kuhakikisha tatizo la umeme linakuwa historia, ndio hayohayo na watendaji wa shirika wamebeba?" alihoji Makonda.

Makonda pia alisema kuwa mwakani, chama hakitamwonea haya mtumishi wa umma kwa uzembe, rushwa au kukiuka maadili ya kazi.

Alisema chama hakifurahishwi na hali ya mgawo wa umeme unaoendelea, kinaona adha wanayoipata wananchi na jambo hilo si la kumwachia Rais au Waziri wa Nishati tu.

Makonda pia aliagiza kuwa kuanzia mwakani, kila wizara itatakiwa kutoa ripoti ya utendaji wake wa kila robo mwaka ili kuonesha namna ilani ya chama inavyotekelezwa.

Mwenezi huyo pia aliwaomba wananchi kuendelea kutoa maoni kwa ajili ya uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 kwa manufaa ya nchi, huku akitangaza kutakuwa na ziara maalum ya viongozi wa chama katika mikoa 10 kuanzia Januari 13 mwakani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa akiwapa pole wazee alipohani msiba wa aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mbekenyera, Mzee Khalid Chikomena, Ruangwa mkoani Lindi jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Matobo 10 miswada Sheria Uchaguzi, vyama vyaja juu

**Na Waandishi Wetu**

KAMATI Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo imesema imebaini miswada ya Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa iliyowasilishwa bungeni na serikali na kusomwa kwa mara ya kwanza Novemba mwaka huu, ina upungufu na kwa sehemu kubwa haiakisi mapendekezo ya wadau wa demokrasia.

Jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alitangaza hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maazimio ya Kamati Kuu ya chama hicho iliyoketi Desemba juzi.

Shaibu alisema Kamati Kuu imeainisha masuala 10 ya kipaumbele ambayo ni lazima yafanyiwe maboresho kwenye miswada hiyo huku ikibainisha kwamba iwapo maeneo hayo hayatafanyiwa kazi, miswada hiyo itapoteza maana yake na kuiathiri falsafa ya '4R' ya Rais Samia Suluhu Hassan yenye lengo la kufungua ukurasa mpya wa kisiasa nchini.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni pamoja na Tume Huru ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, Tume ya Uchaguzi kuwa na watendaji wake watakaosimamia uchaguzi badala ya wakurugenzi wa halmashauri, viongozi wakuu wote wa tume (Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Makamishna na Mkurugenzi wa Uchaguzi) wapatikane kwa kufanyiwa usaili na Kamati ya Usaili kabla ya kuteuliwa na Rais.

Mengine ni kuboresha muundo wa Tume ya Uchaguzi kulingana na maoni ya wadau wa demokrasia ili kuihakikishia uhuru wake ikiwamo wajumbe wa tume kutoondolewa ofisini kwa urahisi, kuboresha kamati ya uteuzi kulingana na mapendekezo ya kikosi kazi na kuweka utaratibu mpya wa ruzuku kulingana na mapendekezo ya kikosi kazi.

Shaibu aliainisha maeneo mengine kuwa ni pamoja na kupunguza madaraka ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuongeza uhuru wa vyama katika kujiendesha, kuongeza uhuru wa kibajeti wa Tume ya Uchaguzi, bajeti ya tume itoke Mfuko Mkuu (Hazina) na si kutoka katika bajeti ya serikali, kuweka masharti kwa vyama ya kiwango maalum cha ushiriki wa wanawake kwenye vikao vya uamuzi na ufanyike kwa mabadiliko madogo ya katiba ili kuiwekea miswada hiyo msingi madhubuti wa kisheria.

Pia alisema Kamati Kuu imeona hakuna namna ya kuepuka mchakato wa Katiba Mpya, ni lazima uanze sasa na serikali inapaswa kuweka wazi ratiba ya mchakato huo.

Sambamba na hilo, Shaibu alisema Kamati Kuu imeiagiza Kamati ya Uongozi Taifa kushirikiana na wadau wote wa demokrasia nchini kuweka shinikizo kuhakikisha miswada iliyowasilishwa, inafanyiwa maboresho kuakisi maoni ya wadau ili kuimarisha uhuru wa kisiasa nchini na kuhakikisha uchaguzi unaofuata unakuwa huru na haki na wa kuaminika.

"Kamati Kuu pia imesikitishwa na mwenendo usioridhisha wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na kuelekeza hatua kadhaa madhubuti za kuchukua. Taarifa juu ya hatua hizo itawasilishwa wakati mwingine," alisema Shaibu.

**KAULI YA CCM**

Wakati ACT-Wazalendo wakiibuka na hoja hizo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, kimesema marekebisho kwenye Sheria ya Tume ya Uchaguzi ni muhimu na tayari Rais Samia Suluhu Hassan amewaomba wananchi washiriki katika utoaji wa maoni.

"Vyama vinavyosema muswada huo una matundu, matobo, haujakamilika. Vyama hivyo vinapaswa kuheshimiwa kwa mawazo yao na kutambua ya kwamba ndio sababu ya kuomba maoni ya wananchi. Kama ulikuwa hauna matobo, tusingeomba maoni ya wananchi.

"Kama haukuwa na upungufu kwanini Bunge litoe muda wa kupokea maoni ya wananchi? Hivyo, ni pongezi kwa serikali yetu, Rais Samia ameridhia taratibu zote za kukamilisha sheria zifuatwe," alisema.

Makonda alisema kwenye siasa ni lazima ujenge hoja na ushawishi na maana ya demokrasia 'wengi wapewe', hivyo msimamo wa chama ni kwamba jambo hilo liko katika utaratibu. Ule upungufu ulioonekana ni wakati wa kuuziba na kutoa mapendekezo mbadala ili wafike kwenye hatua inayostahili.

Alisema katika hilo hakuna sababu ya kusigana, bali wanahitaji kuwa pamoja na kushauriana, ndio kilie alichokiita serikali imekubali kuingia katika mchakato.

Kuhusu maridhiano, Makonda alisema anayedai hakuna dhamira ya maridhiano, anashindwa kumwelewa kwa kuwa mapendekezo ya kubadili sheria ni matokeo ya maridhiano.

"Mikutano ya hadhara inayofanyika si matokea ya maridhiano? Viongozi wa kisiasa waliokuwa na kesi na kufutiwa kesi zao si matokeo ya maridhiano? Mbona tunasahau mapema?

"Usitake kuonekana maridhiano ni yale unayoyataka wewe ndio yawe maridhiano ila ya wenzako si maridhiano, hapana! " alisema Makonda.

Makonda alisema wapinzani ambao yeye tangu aingie madarakani hivi karibuni amekuwa anawaita watoa taarifa, wasipofanya mikutano ya hadhara thamani yake inapotea.

"Thamani yangu inaongezeka kunapokuwa na mikimiki kule. Kama wakitulia ina maana ninashindana mwenyewe... wenzangu siwaoni nimepiga ziara moja siwaoni, naomba niwaalike mwaka 2024 twendeni kazini jamani, tunakula ruzuku za watu twendeni mitaani, twendeni tukafanye mikutano.

"Tusingetamani kuona polisi wakiwasumbua ndugu zetu. Wakifanya mikutano, wapewe ulinzi uliokamilika, wafanye mikutano yao kama wanavyotaka wao, huko ndiko kujenga demokrasia na mimi sipo kwa ajili ya kupambana na mtu, tunashindana kwa hoja," alisema Makonda.

**-Imeandaliwa na Julliet Mkireri na Beatrice Shayo**




Katibu wa Ukuzaji wa Maadili Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Waziri Kipacha (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) ofisini kwake jijini Dodoma jana, kuhusu idadi ya watumishi wa umma waliojaza fomu za tamko la rasilimali na madeni yao. Kulia ni Mkurugenzi Kitengo cha Teknolojia ya Habari (TEHAMA), Stanslaus Mwita na Katibu Msaidizi Idara ya Usimamizi wa Maadili, Sigolwike Mkamati. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

KASHFA ULAJI BIL 8.9/-

# Kesi ya watumishi Dar mbioni kuhamishiwa mahakama kuu

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayowakabili wafanyakazi 15 wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, wanaotuhumiwa kuisababishia halmashauri hiyo hasara ya Sh. bilioni 8.9, umeieleza mahakama kuwa uko kwenye hatua za mwisho kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kwa ajili ya hatua nyingine.

Wafanyakazi hao ambao wanawakilishwa na mawakili zaidi ya kumi, wanashtakiwa kwa makosa 143 ambayo ni pamoja na kuongoza genge la uhalifu, matumizi mabaya ya madaraka, kuingiza taarifa za uongo kwenye mfumo, ufujaji na ubadhirifu, kughushi, utakatishaji fedha na kusababishia hasara.

Wakili wa Serikali, Roida Mwakamele alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa wapo kwenye hatua za mwisho za kupeleka taarifa ya kesi hiyo Mahakama Kuu.

Kutokana na maelezo hayo, Hakimu Ruboroga aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 22, mwakani kwa ajili ya kutajwa. Jopo la mawakili wa utetezi likiongozwa na Wakili Hassan Sinjo na Ramadhani Rashid halikuwa na pingamizi juu ya ahirisho hilo.

Wafanyakazi hao ni: Ofisa Mtendaji wa Kata, Khalid Nyakamande (34); Ofisa Afya, Patrick Chibwana (40); Karani wa Fedha, Judica Ngowo (51); Tulusubya Kamalamo (53); James Bangu (57) na Mohamed Khais (41).

Wengine ni Abdallah Mlwale (52), Deogratias Lutaza (55), Febronia Nangwa (44), Grory Eugen (46), Said Bakari (37), Josephine Sandewe (48), Dorica Gwichala (45), Jesca Lugonzibwa (53) na Ally Baruani (38), wote wakazi wa Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai Mosi, 2019 na Juni 30, 2021, washtakiwa hao waliongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. bilioni 8.9.

Katika shtaka la matumizi ya madaraka, washtakiwa wote 15, wakiwa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa nyadhifa mbalimbali, walishindwa kuingiza mapato katika akaunti za NMB, CRDB, NBC na DCB zinazomilikiwa na jiji na kusababisha hasara ya Sh. 8,931,598,500.

Katika shtaka la kuingiza taarifa za udanganyifu kwenye mfumo, Ngukah alidai kuwa shtaka hilo linawakabili Ngowo, Nangwa na Bakari ambao wanatuhumiwa kulitenda kati ya Julai Mosi, 2019 na Juni 30, 2021.

Inadaiwa kuwa katika shtaka la ufujaji na ubadhirifu linawakabili Kamalamo, Bangu, Khais, Mlwale, Lutaza, Ngowo, Nangwa, Eugen, Bakari, Sandewa na Lugonzibwa ambapo wanatuhumiwa kutumia fedha za halmashauri hiyo kwa maslahi yao binafsi.

Inadaiwa kuwa shtaka la kughushi linawakabili Kamalamo, Bangu, Sandewa, Gwichala, Lugonzibwa, Chibwana, Baruani na Nyakamande.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo Julai Mosi, 2019 wakiwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wanatuhumiwa kuisababishia hasara mamlaka husika Sh. bilioni 8.9.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka hayo, hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi.

## Polisi wajichunguza kwa tuhuma za ukatili kwa raia

**Na Restuta James**

JESHI la Polisi limeanza kuwachunguza maofisa wake wanaotuhumiwa kufanya ukatili kwa raia na kutoa rai kwa watu wenye ushahidi kulisaidia ili uchunguzi ukamilike haraka kwa hatua zaidi za kisheria.

Taarifa ya Msemaji wa Jeshi la Polisi, SACP David Misime, kwa vyombo vya habari jana, ilieleza kuwa baada ya kuona video za wananchi wawili wakilalamika kufanyiwa vitendo vilivyo kinyume cha sheria na haki za binadamu, wamechukua hatua.

SACP Misime aliwataja wananchi waliolalamika kwenye video hizo kuwa ni Getrude Masanja wa Kilimanjaro na Kalamba wa Dodoma.

"Ili kuhakikisha haki inatendeka, Jeshi la Polisi litashirikisha wataalamu wengine wa haki jinai kuchunguza malalamiko hayo, hivyo mwenye ushahidi kulingana na malalamiko yaliyowasilishwa na walalamikaji asisite kujitokeza ili uchunguzi huo ukamilike mapema ili hatua nyingine za kisheria zifuate," alisema Misime katika taarifa hiyo.

Wakati huohuo, SACP Misime amewataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto kwa kuwalinda, kuwajali, kuwasikiliza na kuzungumza nao ili kuwaepusha na vitendo vya unyanyasaji kijinsia.

"Tunatoa wito kwa sababu uzoefu umetuonesha kipindi cha likizo ndefu kama hizi kuna jamii zinaendesha tamaduni potofu kama ukeketaji.

"Pia katika vituo vya polisi kunaripotiwa vitendo vya unyanyasaji kwa watoto vikiwamo vya ubakaji, ulawiti, ukeketaji, kuumizwa, vipigo, kubaguliwa na kuozeshwa katika umri mdogo," alisema SACP Misime.

Alitoa rai kwa viongozi wa serikali za mitaa kushirikiana na polisi kata, wabuni mikakati endelevu ya kuzuia unyanyasaji dhidi ya watoto katika kipindi cha likizo ndefu.

"Tukishirikiana sote kuanzia ngazi ya familia na kwa kila mmoja kwa nafasi yake, watoto wetu watakuwa salama na wenye afya nzuri ya mwili na akili," alifafanua.

# Manufaa makubwa mradi wa bomba mafuta kwa wazawa

**Na Restuta James**

MRADI wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Chongoleani, Tanga (EACOP), umetajwa kuwa na manufaa mengi ikiwamo kuzijengea uwezo kampuni za ndani, kuajiri zaidi ya Watanzania 3,000 na kuandaa wataalamu wa kuusimamia utakapokamilika.

Aidha, mradi umeboresha kilimo kwa kuwapa wananchi wataalamu wa kilimo na mifugo ambao wanawafundisha mbinu bora ili kupata mazao mengi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa EACOP, Catherine Mbatia, alisema mradi huo umeajiri Watanzania kuanzia ngazi ya kijiji unakopita hadi wenye utaalamu.

Mbatria alisema ili kuwajengea uwezo wa kitaalamu Watanzania, EACOP imeingia makubaliano ya mafunzo na vyuo vya ufundi stadi (VETA) ili kuweka masomo maalumu kuhusu uendeshaji wa mradi huo.

"Mradi unazingatia Sheria ya Kulinda Haki za Wazawa ya Mwaka 2017, kwa hiyo umetoa fursa za ajira, mafunzo, kuzijengea uwezo kampuni za ndani na kuhakikisha tunanunua huduma na bidhaa za ndani," alisema.

Aliongeza kuwa tayari wamekwishapokea mabomba yenye urefu wa kilometa 100 za mradi ambayo yatafanyiwa maboresho ili kukidhi viwango vya kutumika.

"Maendeleo ya mradi ni mazuri tumegawa nyumba 399 kwa waathirika waliochukuliwa makazi. Kwa ambao wamechukuliwa mashamba na wakaomba kulipwa fedha, asilimia 99.8 wameshalipwa," alisema Mbatia.

Awali, Mkuu wa Idara ya Fursa kwa Wazawa wa EACOP, Neema Kweka, alisema: "Tunatamani katika miaka mitano ijayo tutakapoanza uendeshaji tusiajiri watu kutoka nje bali Watanzania wawe wamejengewa uwezo ndiyo maana tumeingia makubaliano na VETA ili kuzalisha wataalamu wa kutosha."

Ofisa Mawasiliano wa EACOP, Abass Abraham, alisema maboresho yanayofanywa kwenye mabomba ni pamoja na kuyawekea kifaa maalumu cha kutoa taarifa pale inapotokea hitilafu au mtu kulisogelea kwa kuchimba lilipofukiwa.


Kuhusu kilimo na ufugaji, alisema kwenye vijiji bomba linakopita, wananchi wamepata nafasi ya kupatiwa mbinu za kisasa ili wafuge na kulima kitaalamu.

"Tunawapimia udongo, tunawapa mbegu na mbolea na kwa msimu mmoja tunawalimia shamba. Kwa wafugaji tumewajengea mabanda ya kisasa na kuwapa mbinu bora za ufugaji. Unaweza kuona kwamba EACOP ni fursa ya kubadilisha maisha," alisema.

Mradi wa EACOP una urefu wa kilometa 1,443 na unamilikiwa kwa ubia na kampuni ya Total Energies yenye asilimia 62 ya hisa, serikali ya Tanzania (asilimia 15), Uganda (asilimia 15) na kampuni ya China (asilimia nane).

Mradi huo una kambi 16 ambazo namba moja hadi nne ziko Uganda na namba tano hadi 16 ziko Tanzania na unapita katika mikoa minane na wilaya 24 nchini.

## HABARI KITAIFA




Meneja Masoko wa ALAF Limited, Isamba Kasaka, akikabidhi hundi kwa Violeth Obimbo (kulia), mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ikiwa ni udhamini wa masomo ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili. Wengine kutoka kushoto ni Mkurugenzi Udhibiti Ubora wa UDSM, Prof. Pendo Malangwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Prof. Shani Mchepange. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wengi wa umma bado kuwasilisha matamko ya mali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIONGOZI wa umma 2,475 kati ya 15,762 wamewasilisha tamko la rasilimali na madeni kwa Kamishna wa Maadili ikiwa ni sawa na asilimia 16 ya viongozi wanaopaswa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Katibu Ukuzaji wa Maadili Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Waziri Kipacha, alisema hayo jana wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jijini hapa.

Kipacha alisema hadi kufikia juzi, viongozi 2,475 ndio waliowasilisha matamko yao kuhusu rasilimali na madeni.

"Hadi kufikia jana (juzi) Desemba 20, mwaka huu, viongozi wa umma 2,475 kati ya viongozi 15,762 ndio waliowasilisha tamko la rasilimali na madeni kwa Kamishna wa Maadili. Hii ni sawa na asilimia 16 ya viongozi wote wanaotakiwa kuwasilisha matamko yao kwa mujibu wa sheria," alisema.

Pia alibainisha kuwa zimebaki siku 10 kufika tarehe za mwisho ya viongozi hao kutakiwa kuwasilisha matamko hayo kwa Kamishna kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya Mwaka 1995," alisema.

Kadhalika, aliwakumbusha viongozi wote wa umma kuzingatia matakwa ya Katiba na sheria hiyo ya maadili kuwasilisha tamko na madeni kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Alisema kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, wameanza kupokea matamko kwa njia ya mtandao kwa kiongozi ambaye atashindwa kufika kwenye ofisi zao.

Kipacha alisema ujazaji wa fomu kwa njia hiyo utawezesha viongozi kujaza fomu hizo kwa urahisi zaidi popote pale walipo iwe ndani au nje ya nchi na unapunguza gharama.

"Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kifungu cha 9 (1) (b) kinamtaka kiongozi wa umma kila mwisho wa mwaka kabla ya Desemba 31, kuwasilisha tamko lake kwa Kamishna wa Maadili linaloonyesha rasilimali zake au mume au watoto wake wenye umri usiozidi miaka 18 ambao hawajaoa au kuolewa," alisema.

Aliongeza kuwa viongozi wapya wanapaswa kuwasilisha taarifa zao ndani ya siku 14 baada ya kuteuliwa au kupandishwa cheo.

"Kwa kipindi cha mwaka jana, viongozi 193 hawakurejesha matamko yao na kupewa barua za kutakiwa kujieleza kuhusu sababu zilizowafanya kushindwa kuwasilisha matamko yao lakini 192 walijieleza na mmoja alishindwa na kufikishwa mbele ya Tume ya Maadili," alisema.

Kifungu cha 19 cha Sheria ya Maadili ya kinaipa Sekretarieti ya Maadili kupokea taarifa na tuhuma za ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma, kupokea matamko ya rasilimali na madeni yanayotakiwa kutolewa na viongozi hao pamoja na kufanya uhakika wa matamko yaliyotolewa.

Alisema alisema majukumu mengine ya sekretarieti hiyo ni kutoa elimu ya maadili kwa viongozi hao, kufanya tafiti kuhusu hali ya maadili nchini na kuweka mikakati ya kukuza maadili nchini.

# Benki Dunia yaipatia Tanzania tril. 2.8/-

**Na Maulid Mmbaga**

BANKI ya Dunia (WB) imeipatia Tanzania msaada wa dola milioni 1,135 za Marekeni (sawa na Sh. Trilioni 2.8) kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali ikiwamo ya Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP) ili kuboresha huduma na ustahimilivu wa hali ya hewa.

Taarifa iliyotolewa jana, ilibainisha kuwa wakurugenzi watendaji wa benki hiyo waliidhinisha Ufadhili wa Sera ya Maendeleo (DPF) yenye thamani ya dola milioni 750 ili kusaidia sekta binafsi na dola milioni 385 kwa awamu ya pili ya mradi wa DMDP mwaka huu.

Makamu wa Rais wa WB Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa, alisema mpango wa pili wa ufadhili wa sera ya maendeleo ya kukuza uchumi Tanzania, utawezesha ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) katika kutatua changamoto za muda mrefu ambazo zimekwamisha ukuaji wa uchumi.

Alisema sera hiyo itasaidia pia kutoa msukumo mkubwa kwa mageuzi yanayoendelea ambayo yanalenga kuboresha hali ya biashara, kuimarisha usimamizi wa SOE, kuboresha uwazi na kukuza uthabiti wa kiuchumi.

"Tunaipongeza Tanzania kwa kupitisha mageuzi ili kukuza ukuaji shirikishi zaidi unaoendeshwa na sekta binafsi na ustahimilivu, huku ikikabiliana na changamoto zinazoletwa na matukio ya kimataifa ambayo hayajawahi kushuhudiwa.

"Tumejitolea kuiunga mkono Tanzania katika kuimarisha mageuzi yatakayowezesha ufufuaji wa haraka wa uchumi na kuimarisha misingi ya ukuaji endelevu wa uchumi shirikishi na uthabiti," alisema Kwakwa.

Aliongeza kuwa tathmini ya mkataba wa uchumi, utendaji na kitaasisi zilizotolewa hivi karibuni, zinaonyesha kuwa kuna changamoto kadhaa zinazozuia ukuaji wa sekta binafsi.

Alisema changamoto hizo zinajumuisha mahitaji ya leseni ili kuanzisha na kuendesha biashara, ufikiaji mdogo wa mikopo na madeni ya gharama kubwa ya sekta ya umma pamoja na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani.

Pia alisema tathmini zinaonyesha kuwa ni muhimu kukamilisha msukumo wa uwekezaji wa umma na sera madhubuti za kijamii ili kukuza ujumuishaji na ustahimilivu wa uchumi. Na kwamba DPF inalenga kusaidia kukabiliana na changamoto hizo.

Mkurugenzi wa WB Tanzania, Nathan Belete, alisema: "Tanzania bado iko katika hatari kubwa ya kukabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa na ina uwezo mdogo wa kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza."

Alisema kutokana na changamoto hizo, DMDP awamu ya pili inalenga kuimarisha zaidi Dar es Salaam huku ikiboresha uhamaji, uhai na ustahimilivu.

Salimu Bakari, mkazi wa Tabata Dar es Salaam, alisema mradi wa DMDP utasaidia kwa kiasi kikubwa wakazi wa mkoani hapo kuondokana na athari za mafuriko ambazo zimekuwa zikishuhudia kwa miaka kadhaa inapofika nyakati za mvua.

# Spika mstaafu Job Ndugai alia mtoto wa kiume kutengwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Mstaafu, Job Ndugani, amesema juhudi kubwa zinazofanywa kwa ajili ya kumwezesha mtoto wa kike nchini zimesababisha mtoto wa kiume kutelekezwa.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) wa Dodoma, Ndugai alisema hali hiyo inatishia ustawi wa mtoto wa kiume na kumweka katika mazingira magumu.

"Nilichotaka kusemea ni hatima ya mtoto wa kiume katika nchi yetu sasa. Mimi siishii miaka minane na kwenda hata miaka 20 iliyopita. Mtakumbuka kutoka Beijing (China) tumejishughulisha sana na mtoto wa kike na pia tukajishughulisha sana na mwanamke. Kwa kweli ukitazama matunda ya juhudi hizo, yamekuwa makubwa na ni mazuri yanamfurahisha kila mtu kwa sababu sote tuna watoto wa kike na wa kiume.

"Lakini hivi sasa utaulizwa ni mtu yeyote shule za mtoto wa kike hata kama ni binafsi utataja hii, hii na hii. Ukiulizwa shule za mtoto wa kiume nzuri hata kama ni za binafsi utachukua muda sana kujua ni ipi," alisema.

Ndugai alisema mtoto wa kiume jamii imwacha na kusababisha kuwa chokoraa, 'panya road', kwenye dawa za kulevya na wengi wao kufungwa magerezani.

"Sizungumzii habari ya serikali. Sisi kama jamii tumewaacha watoto wa kiume katika hali mbaya. Ukiwalinganisha watoto wa kiume na wa kike hata ukitembelea shule, utaona tofauti kubwa sana kati yao.

"Ukifika pale shuleni watoto wakaja pale labda mwalimu amekuruhusu wamekuja ukiwatazama utaona watoto wa kiume wanarudi nyuma watoto wa kike ndio wanakuja mbele. Lakini kwa wale manaokwenda kanisani, kwaya zilizoko pale kama ni wanakwaya 40, wanaume wawili au watatu, 35 na zaidi ni wasichana," alisema.

Katika kila shughuli, alisema wanawake wako mbele hata matokeo ya shule ya kitaifa sasa hivi watoto wa kike wanafanya vizuri zaidi.

"Si jambo baya ni jambo zuri lakini utaona kwamba watoto wa kike hata walioishia darasa la saba wanajitambua wanakwenda hata kufanya kazi za ndani ili tu wapate chochote kitu. Hawa wa kiume wako kwa mama zao wanasubiri wale ugali kwa mama zao.

"Wanakwenda kucheza 'pool' na kurudi, yaani hawana mwelekeo hata wawe wamemaliza chuo kikuu. Pamoja na diploma, mtoto wa kike atajishughulisha, mtoto wa kiume yupo yupo tu analelewa na mama yake," alisema.

"Hata vijijini wabunge mkiangalia unaita mkutano wa hadhara we tazama mkutano wako wa hadhara ulivyoangalia kundi la wanawake na kundi la wanaume, utakuta kundi la wanawake angalau wamevaa vizuri. Tazama wale wanaume walivyochakaa, yaani kabisa naongelea ukweli. Watoto wa kiume hawako vizuri na sisi kama jamii hatulioni hili.

"Unategemea hawa waje waone nani kwanza vijijini kule siku hizi ndoa ziko ngapi kwa mwaka. Kijiji kizima ndoa kama zinazidi tatu kwa mwaka ni bahati," aliongeza.

Ndugai alisema kwa hali halisi ya sasa, hakuna vijana wa kiume wa kuoa kwa hiyo tatizo hilo linatakiwa kupelekewa jicho kidogo kwa mtoto wa kiume na kama taifa, vinginevyo mzani wa usawa wa kijinsia umekuwa na tatizo.

Alisema juhudi za mtoto wa kike ziendele kama kawaida lakini mtoto wak uje asisahauliwe, hivyo linapozungumzwa suala la jinsia, mtoto wa kiume pia akumbukwe badala ya mzani kuelemewa kwa mtoto wa kiume pekee.

# NMB yatoa zawadi washindi 100 kampeni ya MastaBata

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetangaza washindi 100 wa droo ya saba ya kampeni yake ya 'MastaBata Halipoi' iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumza wakati wa droo hiyo iliyofanyika Mbagala, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mbagala, Halima Mcharazo, alisema washindi 100 wa benki hiyo watapata zawadi ya fedha taslimu 100,000/- kila mmoja na kuongeza kuwa kampeni ya miezi mitatu ya benki hiyo inalenga kuwashukuru wateja wa benki hiyo kwa kuendelea kuwa na imani na benki hiyo.

Mcharazo alibainisha kuwa zaidi ya wateja 620 hadi sasa wamebahatika kujishindia zawadi za fedha taslimu wakati wa droo za kila wiki na mwezi wakati wa kampeni ya benki hiyo ya MastaBata iliyozinduliwa mnamo Oktoba 27, 2023.

"Msimu wa kutoa umewadia na unatupa fursa nyingine ya kuonesha upendo na shukrani zetu kwa wateja wetu. Kupitia droo ya kampeni yetu ya MastaBata, leo (jana) wateja wetu 100 watakaobahatika watajishindia Sh. 100,000 kila mmoja," alisema.

Mcharazo alisema kampeni hiyo inayotarajiwa kufika kilele Januari 25, 2024, itawawezesha wateja wa benki hiyo kujishindia zawadi za zaidi ya Sh. milioni 350 za fedha taslimu na safari za mapumziko mwisho wa mwezi katika fukwe za Kendwa Rocks visiwani Zanzibar na safari za Cape Town, Afrika Kusini katika droo ya mwisho wa kampeni.

"Kampeni yetu inalenga kuhamasisha malipo ya kidijitali ambayo yameonekana kuwa rahisi zaidi, ya haraka na salama.

"Kwa mantiki hiyo, ninawahimiza wateja wetu wa Benki ya NMB kuendelea kutumia kadi zao za MasterCard wanapolipia bidhaa au huduma kupitia Mashine za Malipo (POS), QR Code au ununuzi wa mtandao ili kupata nafasi ya kushinda fedha taslimu na safari zilizogharamiwa kila kitu na benki wakati wa kampeni," alisema.

Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Irene Kawili wakati wa hafla hiyo alibainisha kuwa droo ya kampeni ya MastaBata inafanyika kwa kuzingatia kanuni na taratibu za bodi hiyo.

"Kampeni ya MastaBata inaendeshwa kwa uwazi sana. Ninawahimiza wateja wa benki kuendelea kutumia njia za kidijitali za malipo ya benki ili kuongeza nafasi zao za kushinda," alisema.



Mkazi wa Mabibo, Hemedi Abdalla, akiangalia nyumba anayoishi na anakofanyia biashara jinsi kulivyobomolewa na maji ya mvua na kuwa sehemu ya bonde eneo la Mabibo Darajani, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mahindi yaharibiwa kwa sumu shambani

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linawatafuta watuhumiwa wa kosa la kuharibu mali katika kijiji cha Halungu-Mbozi.

Taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Theopista Mallya, ilibainisha kuwa mnamo Desemba 18, mwaka huu, huko kata ya Halungu, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, shamba la mahindi lenye ukubwa wa heka 11 lililolimwa na watu wanne walilokodi kwa Edina Mgala, liliharibiwa baada ya kupuliziwa dawa inayopdhaniwa ya kuulia magugu na mtu/watu wasiofahamika.

Kamanda Theopista alibainisha katika taarifa yake hiyo kuwa shamba hilo lilikodishwa kwa kuligawa kwa watu hao wanne; Mailo Msangawale (35) ekari saba, Emi Magwaza (48) ekari 1.5, Salome Nkota (50) ekari 1.5 na Jeremia Ngoya (42) ekari moja, wote wakulima na wakazi wa Halungu.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa ardhi unaohusisha familia mbili kati ya watoto wa mke mkubwa na mke mdogo wa marehemu Focus Makonongo.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kwa kushirikiana na maofisa kilimo wilaya ya Mbozi linafanya tathmini ili kujua thamani halisi ya mali iliyoharibiwa pamoja na kemikali iliyotumika kufanya uharibifu huo.

"Jeshi la Polisi mkoa wa Songwe linatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za mtu au watu ambao wamehusika katika tukio hilo ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Aidha Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe linatoa rai kwa wananchi kutokujichukulia sheria mkononi badala yake kutatua migogoro kwa kukaa vikao na kusuluhisha kwa amani," Kamanda Mally alibainisha katika taarifa yake hiyo.


ANATAFUTWA



DEO THADEI FUMBE

ANATAFUTWA NA MWAJIRI WAKE KWA KOSA LA WIZI.
**RB NAMBA MOR/RB/11400/2023¬**

MWENYE TAARIFA YA MAHALI ALIPO ATOE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE AU **PIGA SIMU NAMBA 0768099480.**

ZAWADI NONO ITATOLEWA

117766502

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la dawa, vifaa tiba bandia lisifanyiwe mzaha

**KASI** ya kukamatwa kwa dawa bandia au zilizoisha muda wa matumizi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kasi hiyo inajidhihirisha kutokana na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), kukamata mara kwa mara katika mikoa mbalimbali nchini.

Hivi karibuni kwa mfano, mamlaka hiyo ilitangaza kukamatwa kwa dawa zisizosajiliwa zenye thamani ya Sh. milioni 133.3 katika mikoa 13 kupitia operesheni maalum ya kukamata dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya serikali, bandia, duni, zisizo na usajili na dawa za kulevya iliyofanyika Novemba, mwaka huu.

Kutokana na operesheni hiyo iliyosababisha kukamatwa kwa dawa hizo, mamlaka hiyo kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu, Adam Fimbo, faini za Sh. milioni 100 zilikusanywa huku majalada 13 yakiwa yamefunguliwa dhidi ya watuhumiwa wakati taratibu za kuwafikisha mahakamani zikiendelea.

Fimbo katika taarifa hiyo, alisema katika operesheini hiyo iliyohusisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kilevya (DCEA), Baraza la Famasia, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa ma Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Jeshi la Polisi katika mikoa ya Dar es Saam, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Katavi, Mwanza, Simiyu, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Songwe, Lindi na Ruvuma, pia vilikamatwa vifaa tiba na vitendanishi ambavyo havijasajiliwa na kutambuliwa vikiwa na thamani ya Sh. milioni 17.7 katika kanda zote.

Sambamba na dawa hizo, vitendanishi na vifaa tiba, pia zilikamatwa dawa zenye madhara ya kulevya aina ya Pethidine kwenye maeneo mbalimbali zikiuzwa kwa siri na mtandao wote ulibainika na wahusika kufahamika.

Aidha, vilikamatwa vifaa tiba vilivyoisha muda wa matumizi vyenye thamani inayokadiriwa kuwa Sh. milioni 10.3 vikiwa havijatengwa kwa mujibu wa taratibu pamoja na dawa bandia za binadamu zenye thamani ya Sh. milioni 5.9 katika Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Magharibi.

Kwa ujumla, taarifa za kukamatwa kwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi hivyo pamoja na dawa za kulevya, haileti picha nzuri kwa mamilioni ya Watanzania.

Kwa maneno mengine, afya za Watanzania wengi ziko hatarini kutokana na kasi ya kusambaa kwa dawa na vifaa tiba hivyo. Ni wazi kwamba hali iko hivyo kwa sababu ni Watanzania wangapi wanaotambua kuwa dawa hizo ama hazijasajiliwa au zimekwisha muda wa matunmizi, hivyo ni hatari kwa afya zao?

Operesheni iliyofanywa na TMDA kwa kushirikiana na wadau wengine ni ya kupongezwa kwa kuwa imeanika mambo yanayopendekezwa katika sekta ya afya hususan eneo la dawa na vifaa tiba. Pamoja na pongezi hizo, kuna jambo la kujiuliza kwa nini jambo hili lifanyike kwa msimu ilhali maisha ya Watanzania yakiendelea kuwekwa rehani kwa kuwapo kwa dawa bandia na zilizokwisha muda wa matumizi?

Ni dhahiri kwamba watu waliopewa dhamana katika usimamizi na ukaguzi wa dawa na vifaa tiba wana upungufu katika utekelezaji wa majukumu yao, hivyo wanapaswa kujiangalia na kujitathmini kwa kuwa wana jukumu zito katika kulinda afya za Watanzania.

Kama alivyosema Msajili wa Bodi ya Famasia, Elizabeth Shekalaghe, kuwa wataalamu walioko kwenye maeneo ambayo dawa na vifaa tiba hivyo vimekamatwa, wamechukuliwa hatua, ni wazi kwamba wameshindwa kutekeleza wajibu wao.

Hilo linaonyesha wazi kwamba kuna tatizo katika utendaji wa baadhi ya watumishi wa umma katika kulinda afya za wananchi.

Ni vyema suala la dawa bandia na zilizokwisha muda lisifanyiwe masihara katika kuhakikisha Watanzania wanatumia dawa na vifaa tiba vilivyothibitishwa ubora wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vurugu, tabia chafu sikukuu, tusioneane aibu

Na Tuntule Swebe

**KATIKA** msimu huu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, wapo waliobaki kwenye sintofahamu wakiwaza, je, nini kitatokea msimu huu? Kwani kila sikukuu vijana na hata watu wazima wa makamo, wanatumia fursa hiyo kutenda uovu kama vile kuwaibia watu na wengine wao kulewa kupita kiasi.

Baadhi wanaunda magenge ya uhalifu kama vile vijana wanaojiita 'panyarodi' tena, nao bila ya woga huwaibia watu mchana kweupe na wengine kuwadhurru watu, kwa lengo la kuambulia maslahi yao binafsi. Ni kilio kikuu kila mtu anataka apate pesa za ama kujikimu au kufurahi maisha na hasa msimu huu.

Kuna watu wengine wanabaki chanzo cha uchochezi wa magenge hayo. Hapo ndio tujiuliza, je unajua magenge hayo yanayo hujidanganya kuwa kipindi hiki cha sikukuu 'ni msimu wa kupiga hela' wanakua kwenye wakati gani, ambao wengine wanawaza wafanye nini waweze kushererekea sikukuu hizo?

Kuna wanaowaza wafanye nini, ili waweze kuwatafutia watoto ada za shule, maana mwaka mpya uko jirani. Wapo kwenye mkanganyiko wa mawazo. Ngoja hili likae wazi, ili kila mmoja atambue nini cha kufanya na nini chaku kukemea, hali ikae shwari.

Kuna baadhi ya kinababa, msimu huu hulewa kupita kiasi na kusababisha ugomvi kwenye familia zao, hali ambayo siyo sahii kabisa, kwani wengine wao huzusha ugomvi unao chochewa na pombe.

Hata kinamama, pia wapo wanaolewa kupita kiasi hadi kuzua ugomvi na wenza wao. Hali hii nayo siyo sawa kabisa, kwani wengine hupigana na wengine wanajeruhiwa, hivyo badala yake wanaanza kuuguza majeraha na kuna matukio, ubaya waje tumeshuhudia kifo wakati mwingine

Hilo linatokana na mjeruhiwa kutokwa damu nyingi, pindi katika ugomvi huo. Hali siyo nzuri kabisa, hivyo tabu huipata watu wa karibu yao.

Inashangaza hata baadhi ya madereva wanalewa kupita kiasi na kujisahau kuwa wao wanaendesha vyombo vya moto, kwani magari ya abiria na ya mtu mmoja mmoja wanapolewa kupita kiasi, madereva hawa husababisha ajali na wakati mwingine tumeona vifo

Baadhi ya kaya hukumbwa na upweke kwa kupoteza wenzi wao kwa ajali au wanaopata majeraha ya kudumu, kukisababisha ongezeko la walemavu kwa ajali.

Kipindi hiki, wengine wao wanakuwa na luga za matusi kwa sababu tu wamelewa, wakigombana na watu hata wasio na uhusiano nao. Vyote navyo vinaleta uchochezi wa fujo na wanyonge kukosa amani.

Je, nini kifanyike? Kwa wanaokwapulia watu au kuunda magenge ya uhalifu, sheria au nguvu ya serikali isimame imara hakikisha watu wanasherehekea sikukuu kwa amani na kuwatia nguvu watu walio kwenye makundi, hata kuwatia nguvu wanaovunja amani.

Ikumbukwe, wapo wenye hatua za mkononi, hivyo mtumie uhuru wenu vizuri na siyo kuwaibia watu na kuhatarisha maisha ya wenzenu. Vilevile, wana - usalama barabarani, wasiwafumbie macho hao wanaolewa kupita kiasi, kisa wanasherehekea siku hizo.

Ni wakati mwingine vitendo vinachangia mikasa ya vifo vya watu. Hao wana watu hawa wachukuliwe, hatua vinasababisha ongezeko la ajali barabarani

Wazazi kipindi hiki cha msimu wa sikukuu wawe kariubu na watoto wao, ili kuwaepusha kwenye makundi ya uhalifu na kuwapa elimu ya makundi ya uhalifu, hata madhara yake na kuwatolea mifano iliyo hai, jambo litakalosaidia kupungua kwa wimbi la uhalifu, hasa kwa nyakati hizi za sikukuu

Naisihi serikali isiwafumbie macho watu wenye lugha chafu kwa kisingizio cha kulewa, kwani hawa wanaipotosha jamii hususani watoto wadogo wanaoiga tabia hizo.

Tujue, watu hawa vichwa vyao ni vyepesi kujifunza lugha hizo zisizo stahili na kuwamezesha watoto lugha hizo.

Wito kwa wazazi na walezi msimu huu wa sikukuu, wasisahau kuwa matumizi yasiyo ya lazima ya fedha wakati wa sikukuu, sio lazima kuyafanya, kwani Januari ijayo kuna ada za atoto shule, pia chakula cha familia nyumbani, bila kusahau mada 'futari ya shule' na akiba kwa ajili ya maradhi, maana magonjwa hayana hodi.

## HABARI KITAIFA

# Naibu Waziri Ardhi atembelea maeneo yaliyoathiriwa maporomoko ya Hanang'

**Na Munir Shemweta,**
HANANG'

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda ametembelea maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko yaliyotokana na maporomoko ya mawe, magogo na tope kutoka Mlima Hanang'.

Pinda alitembelea maeneo hayo juzi kabla ya kuhudhuria kikao cha utekelezaji maagizo kuhusu mafuriko yaliyotokana na maporomoko hayo.

Naibu Waziri Pinda alitembelea maeneo yaliyoathirika kwenye mji wa Katesh na Kijiji cha Gendabi, mkoani Manyara.

Akiwa katika maeneo hayo, naibu waziri huyo alikutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu), Jenista Mhagama aliyekwenda kutembelea maeneo mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kujionea urejeshaji wa hali katika maeneo yaliyoathiriwa na janga hilo.

Wakiwa katika maeneo ya waathirika, mawaziri walijionea hali halisi ya urejeshaji hali katika maeneo yaliyoathirika na maafa na kukagua ugawaji misaada kwa wananchi walioathirika na maafa.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na mawaziri hao, walieleza kuridhishwa na juhudi za serikali hasa Rais Samia Suluhu Hassan katika kusaidia waliokumbwa na athari ya mafuriko katika eneo hilo.

"Tunaomba mtupelekee salamu na shukran zetu kwa Rais Samia kutokana na juhudi zake na jinsi alivyolipa uzito suala hili la waathirika wa mafuriko, tumhakikishie tuko pamoja naye," walisema.

Mafuriko yaliyotokana na maporomoko ya mawe, magogo na tope kutoka mlima Hanang yamesababisha vifo vya watu 89 na majeruhi wanaoendelea kupata matibabu katika hospitali za Hydom, wilaya na mkoa.

Sambamba na hilo baadhi ya wananchi wanaendelea kupata hifadhi katika maeneo ya taasisi za elimu zilizoko Katesh baada ya makazi yao kuharibiwa.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akipita katika moja ya nyumba iliyoathirika na mafuriko ya Hanang jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRC yaongeza safari za treni mikoa ya kaskazini

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limeongeza safari za treni za abiria kutoka Dar es Salaam kuelekea mikoa ya kaskazini, ikigusa mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha.

Mkoani Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji TRC, Focus Sahani, alisema kuongezwa kwa safari hizo kumetokana na ongezeko la abiria wanaosafiri kwa sababu mbalimbali kipindi hiki cha mwisho wa mwaka.

Sahani alieleza kuwa treni kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi na Arusha zitakuwa zinasafirisha abiria siku za Jumatatu, Jumatano na Alhamisi na treni kutoka Arusha na Moshi kwenda Dar es Salaam zitakuwa zinasafiri siku za Jumanne na Alhamisi.

"Kuelekea sikukuu ya Krismasi Desemba 25, mwaka huu na ongezeko la abiria wanaosafiri mikoa ya kaskazini, shirika limeongeza treni ya ziada ambayo itasafiri siku ya Jumamosi Desemba 23 saa 2:00 asubuhi kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi na Arusha," alisema Sahani. Aliongeza kuwa treni hiyo itakuwa na mabehewa 18. Kati yake, tisa ni ya daraja la tatu, manne la pili kukaa na mengine manne daraja la pili kulala.

"Kama shirika tunawajali abiria wetu na Watanzania kwa ujumla, tumeona kuna haja kuongeza treni maalum kwa ajili ya kupeleka watu kula sikukuu Moshi na Arusha," alisema Sahani.

Stanley Msuya, mmoja wa abiria wa treni, alionesha kufurahishwa na hatua ya shirika hilo kuendelea kuboresha usafiri huo kipindi hiki ambacho kuna idadi kubwa ya abiria.

Alisema uamuzi huo unawasaidia Watanzania wengi hasa ambao hawawezi kumudu ongezeko la bei ya mabasi msimu huu wa sikukuu kutokana na hali ya kiuchumi.

"Mimi ni mdau wa treni siku zote. Kwanza, usafiri wa treni ni bei rahisi mno kulinganisha na mabasi na ndege na pia hakuna usumbufu. Ukipanda treni kila kitu unakipata ndani ya treni mpaka mwisho wa safari," alisema Stanley.

Kwa mujibu wa shirika hilo, sasa bei za treni zinazofanya safari kutoka Dar es Salaam mpaka Moshi nauli yake ni Sh. 16,500 daraja la tatu, Sh. 18,100 daraja la pili kukaa na Sh. 39,100 daraja la pili kulala.

Pia safari za kutoka Dar es Salaam hadi Arusha ni Sh. 18,700 daraja la tatu, Sh. 23,700 daraja la pili kukaa na Sh. 44,100 daraja la pili kulala.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Waweka kambi kutibu mtoto wa jicho

**Na Steven William,** MUHEZA

MADAKTARI wa macho kutoka Hospitali ya Mvumi wameweka kambi siku tatu wilayani Muheza, mkoani Tanga kwa ajili ya kutibu wagonjwa wenye tatizo la mtoto wa jicho.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Juma Mombokaleo, alibainisha hayo jana wakati wa ufunguzi wa kambi hiyo katika Kituo cha Afya Ubwari kilichoko Mtaa wa Mbaramo wilayani hapa.

Alisema mpango huo unalenga kuwabaini wagonjwa hao wilayani Muheza, kambi hiyo ikifadhiliwa na Halmashauri ya Muheza na Shirika la Charity Vision na Shirika la Misaada la Mwezi na Jua. Dk. Mombokaleo alisema kambi hiyo ilianza jana na inatarajiwa kuendelea kwa siku tatu ili kubaini wagonjwa wenye tatizo la mtoto wa jicho na kuwafanyia upasuaji.

Alisema huduma zinazotolewa kwa wananchi hao ni kupima macho, kutoa dawa, upasuaji wa mtoto wa jicho na kutoa miwani ya kusomea.

Dk. Mombokaleo alisema madaktari bingwa wanashirikiana katika kufanya upasuaji na wana uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wengi katika kipindi kifupi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina alisema wanaopata ugonjwa wa mtoto wa jicho wengi wao ni wazee na wanakosa watu wa kuwasindikiza kwa kuwa hawaoni.

Alishauri wananchi wilayani Muheza kujitokeza kwa wingi katika huduma hiyo ambayo inatolewa na wataalamu hao bila malipo. Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alishukuru madaktari hao wa macho kutoka Hospitali ya Mvumi kwa kutoa matibabu hayo bila malipo kwa wananchi wa Muheza.




Wakazi wilayani Muheza, Mkoa wa Tanga wakisubiri kuitwa ndani ya chumba maalum cha matibabu ya macho katika Kituo cha Afya cha Ubwari baada ya madaktari bingwa wa macho kutoka Hospitali ya Mvumi kuweka kambi siku tatu wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri Jafo ataka bajeti kwa ajili ya uzalishaji miche

**Na Robert Hokororo,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amezielekeza halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kuzalisha miche ili kuongeza nguvu katika upandaji miti.

Aliagiza hayo jana alipofanya ziara ya kukagua vitalu vya miche inayozalishwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Jiji la Dodoma pamoja na vikundi katika eneo la Mailimbili.

Dk. Jafo alizitaka mamlaka hizo za serikali za mitaa zaidi ya 180 kuwatumia wataalamu wa miti wa TFS ili kuzalisha miche kwa wingi ambayo inahitajika kwa kiasi kikubwa ili kufikia lengo la upandaji miti milioni 1.5 kwa mwaka kwa kila halmashauri.

Pia alielekeza halmashauri kutumia maeneo ya pembezoni mwa barabara kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijiji na Vijijini (TARURA) kuandaa vitalu ili kupendezesha miji.

Waziri Jafo pia aliwataka wananchi kutumia mvua ya vuli inayonyesha katika baadhi ya maeneo nchini kuelekea masika kwa kupanda miti kwa wingi kama ambavyo viongozi wakuu wameelekeza.

"Nimefarijika kutembelea maeneo haya yanayozalisha miche hii ya miti mbalimbali na ninawapongeza sana TFS na vikundi vya kijamii vinavyojishughulisha na uzalishaji wa miche kwani si tu wanasaidia upatikanaji miche, bali pia wamejitengenezea ajira," alisema.

Dk. Jafo alikumbusha maelekezo ya serikali ya kupanda miti yaliyoanzishiwa kampeni mbalimbali ambazo zinahamasisha upandaji miti. Kamishna wa Uhifadhi wa Kanda ya Kati wa TFS, Mathew Kiondo, alihimiza wananchi kujitokeza kwa wingi kuchukua miche ili waipande na kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Alisema pamoja na wakala huo kuzalisha miche na kuigawa bila malipo, kasi ya mwitikio wa uchukuaji miche ni ndogo, akiwa na ufafanuzi kuwa kati ya milioni moja, ni 200 tu imeshagawiwa kwa wananchi.

"Tuna malengo ya kuibadilisha Dodoma kuwa ya kijani na ndio maana ili kuongeza kasi ya uzalishaji miche, tumeanzisisha greenhouse (kitalu nyumba) hivyo tunawaomba mje kwa wingi mchukue miche mkaipande," alisisitiza Kiondo.

Ofisa Mazingira wa Mkoa wa Dodoma, Salvatory Mashamba, aliwaomba viongozi wenzake wa jiji hilo kutenga maeneo ya wazi na kuwagawia wadau ili waandae vitalu. Pia alishukuru TFS kwa utaraibu wao wa kuzalisha miche kisha kuigawa bila malipo kwa wananchi, hatua inayosaidia kuhakikisha upatikanaji miche unakuwa wa uhakika.

# Viongozi CCM Kata ya Tangini walia kufanya vikao vyao baa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Tangini, mjini Kibaha, mkoani Pwani, wameomba wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia ujenzi wa ofisi yao ili waondokane na kufanyia vikao vyao kwenye baa.

Ofisi hiyo hadi kukamilika inahitaji Sh. milioni 60 na hadi sasa iko katika hatua ya msingi ambapo zaidi ya Sh. milioni saba zimeshatumika.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada kutoka kwa kampuni ya Kyem inayojishughulisha na uuzaji wa chuma chakavu, Katibu wa CCM Tangini, Sophia Mtasi, alisema kutokana na kukosa ofisi wanalazimika kufanya kazi zao nyumbani.

Sophia alisema ujenzi kwa sasa unaendelea na unatarajiwa kukamilika Machi mwakani na kwamba matofali 7,000 yanahitajika kujenga jengo hilo ambalo litarahisisha utendaji kazi kwa viongozi na wanachama kupatiwa huduma katika eneo sahihi.

Akikabidhi vifaa katika ofisi ya chama hicho, Mkurugenzi Msaidizi wa Kampuni ya Kyemi, Matha Jackson, alisema wamekuwa wanasaidia makundi mbalimbali katika mji wa Kibaha, baada ya kuombwa msaada na uongozi wa chama hicho, wameitika wito.

Martha alisema wataendelea kushirikiana na uongozi wa chama hicho pale msaada utakapohitajika.

"Jamii inayotuzunguka ndio wadau wetu wakubwa na tumekuwa tunashirikiana nao kwa mambo mengi, misaada tumetoa kwa makundi ya wazee, yatima na wanaotuzunguka sehemu ya kazi, tumeajiri vijana zaidi ya 200 wazawa na sasa tumekuja kutoa kwa ofisi ya chama kufanikisha ujenzi wao," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mailimoja, Shauri Yombayomba, aliishukuru kampuni ya Kyem kwa msaada huo kwa kuwa baada ya kuwafikishia maombi ya ujenzi huo, wameonesha mwitikio wa haraka na kusaidia.

Jeremia Komba, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Kata ya Tangini, alisema ujenzi wa ofisi hiyo utarahisisha utendaji kazi wa viongozi huku akiwapongeza wanaoendelea kutoa michango ya fedha na vifaa.



# FAO yawezesha vifaa vya kulinda mazalia ya samaki

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), limeviwezesha vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Bahari na Pwani (BMU), Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kulinda mazalia ya samaki.

Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi wa Wizara ya Mifugo, Merisia Mpalazo, akizungumza jana katika hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo, alisema wizara inatekeleza maelekezo hayo kupitia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sheria za Uvuvi, kanuni, miongozo pamoja na taratibu nyingine zilizopo. "Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na kutekeleza maelekezo hayo lakini bado tunatambua umuhimu wa kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu.

"Tukiwa sisi wenyewe hatuwezi kuyatekeleza ndiyo maana tunashirikisha halmashauri za wilaya, taasisi zisizo za kiserikali, wadau wa maendeleo wakiwamo hawa wenzetu wa FAO, katika kuhakikisha kwamba tunafikia lengo la kufanya uvuvi uweze kuchangia kikamilifu pato la taifa," alisema.

Aidha, alisema dhana ya ushirikishwaji huo inalenga kuleta uwajibikaji wa pamoja wa wadau wote katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kusimamia rasilimali za uvuvi.

"Sote tunajua kwamba ushirikishwaji wa jamii ya uvuvi ni kupitia hivi vikundi vya rasilimali za wavuvi ambao tunawatumia sana na wanafanya kazi zao vizuri na hawa ndiyo wawakilishi wa wananchi wote walioko kwenye shughuli za uvuvi," alibainisha.

Mtaalamu wa samaki kutoka FAO, Prisca Issangya, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha usalama wa chakula pamoja na kuongeza ushiriki katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali za bahari hususani kwa vijana na wanawake katika jamii za pwani.

Mmoja wa wanufaika wa vifaa hivyo, Sitaruki Bwago, alishukuru shirika hilo kupitia serikali kwa kupata mradi huo ambao utaenda kuwaongezea hamasa ya ufanyaji wa shughuli zao.

Alisema awali walikuwa na tatizo la vifaa duni ambavyo hawakuweza kufanya shughuli zao ipasavyo, lakini matukio ya kihalifu yalijitokeza kutokana na kukosa vifaa kama makoti ya majini, viona mbali, simu maalumu za mawasiliano baharini na vinginevyo ambavyo kwa sasa wamepatiwa.

Bwago aliwataka BMU kuvitunza na kuvitumia vifaa hivyo kwa matumizi yaliyokusudiwa ili viwaletee manufaa katika shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuwatua nguvu FAO kwa kuwaletea msaada huo.



Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mirerani Multipurpose Cooperative Society LTD wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Rose Justo (kushoto), akizungumza kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Misaada yazidi kumiminika kwa waathirika Hanang'

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA cha Kutetea Haki za Watoto mkoani Arusha (ACRO), kimetoa msaada wa vyakula, nguo, vifaa vya shule na fedha kwa waathirika waliokumbwa na mafuriko yaliyoambatana na tope katika eneo la Katesh wilayani Hanang mkoani Manyara.Akikabidhi msaada huo jana kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, Mwenyekiti wa ACRO, Josephat Mmanyi, alisema chama hicho kimeguswa kutoa msaada huo kwa lengo la kuwasaidia Watanzania wenzao wenye shida.

"Tumeguswa kuwasaidia watu wa Hanang' waliokumbwa na maafa, ili waweze kujiona wapo na ndugu zao, ambao ni sisi Watanzania wenzao, tunawaomba wananchi kumuunga mkono Mkuu wa Mkoa wa Arusha ili wenzetu waweze kupata huduma kama ilivyokuwa awali," alisema.

Baada ya kupokea msaada huo, Mongella, aliwashukuru viongozi wa chama hicho kwa kutoa msaada huo kwa waathirika wa mafuriko ya matope.

"Mara nyingi tulizoea wakipita kutaka kushikwa mkono kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, lakini sasa hivi wao wanatoa msaada kwa waathirika wa maafa ya Katesh, hili jambo limedhihirishia usemi usemao kutoa ni moyo na siyo utajiri," alisema Mongella.

Pia aliwataka wananchi mkoani hapa watakaoguswa kutoa msaada wafanye hivyo kwa kuwa bado waathirika wanahitaji msaada.

Alisema serikali ya Mkoa wa Arusha bado inafanya kazi ya kuratibu ili kuhakikisha misaada yote inayotolewa inawafikia walengwa na siyo vinginevyo, kama Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alivyoagiza.

"Tumeelekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa uratibu wa upokeaji misaada ufanyike kwa uwazi ikiwamo kuifikisha kwa waathirika, nitamfikishia salamu za wana ACRO kwa kuwa jambo hili ni funzo kwetu. "Watanzania wote tunapaswa kuiga mfano huu, hata hivyo fedha mlizotoa kwa ajili ya kusafirishia mzigo huu, tutaziwasilisha kwa walengwa kwa kuwa hilo ni jukumu la mkoa kusafirisha misaada itakayotolewa kwa waathirika," alisema Mongella.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgie, aliwashukuru wadau hao kwa msaada huo akisema kuna watoto ambao wameathirika katika eneo la Katesh, hivyo msaada huo utakwenda kuwahudumia.

# Waanzisha kilimo ikolojia kunufaisha mfumo chakula

**Na Allan Isack,** MANYARA

MTANDAO wa Wakulima wa Mkoa wa Manyara (MVIWAMA), umekuja na mpango wa kilimo ikolojia ambao lengo kuu ni kunufaisha mfumo endelevu wa chakula.

Mratibu wa MVIWAMA, Valentin Ngorisa, aliyasema hayo kwenye Mkutano Mkuu wa 16 wa MVIWAMA, uliofanyika mjini Babati.

Ngorisa alisema kilimo ikolojia ni njia ya kilimo inayolenga kuhifadhi na kuheshimu mazingira kwa kuzingatia matumizi endelevu ya ardhi, rasilimali na bioanuwai.

Aidha, alisema kupitia kilimo ikolojia kutazuia au kupunguza matumizi ya kemikali za viwandani na mbolea za kemikali na kuwekeza katika mbinu za kuhifadhi maji kama vile matumizi ya makinga maji.

"Kilimo hiki kinazingatia mzunguko wa asili wa ikolojia kukiboresha afya ya udongo, kudumisha uzalishaji wa mazao bila kutumia kemikali hatarishi na kukuza mfumo wa kilimo endelevu unaolenga kuhifadhi mazingira kwa vizazi vijavyo," alisema.

Mwenyekiti wa MVIWAMA, Paulo Joseph, alisema kilimo ikolojia kinahimiza mifumo inayowezesha wakulima wadogo kuwapatia maarifa na teknolojia.


Joseph alisema kupitia kilimo ikolojia wakulima watatumia mbegu za asili ambazo zinafaa kwa mazingira ya eneo na zinazohimili magonjwa na hali ya hewa ya eneo husika.

Ofisa Ugani wa MVIWAMA, Thomas Joseph, alisema katika kilimo ikolojia kinasisitiza matumizi ya mbolea za asili na siyo kemikali za viwandani.

"Kilimo ikolojia kinapunguza na kuondoa matumizi ya kemikali za dawa za wadudu, ikitegemea zaidi mbinu za asili za udhibiti wa wadudu na magonjwa," alisema Joseph.

Mkulima wilayani Babati, Joyce Elias, alisema kupitia kilimo ikolojia watatumia mbolea ya samadi, mboji na mkojo wa sungura na kuachana na kemikali za viwandani zenye madhara.

Mkulima mwingine kutoka wilayani Kiteto, Samwel Palangyo, alisema kupitia kilimo ikolojia watanufaika na kuendelea kupata mahindi ya asili ambayo ni matamu.





# Polisi yatuma salamu kwa madereva walevi sikukuu Krismas, Mwaka Mpya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewatangazia kiama madereva wazembe na wasiofuata sheria za barabarani na kuahidi kuwachukulia hatua kali za kisheria hususani katika kipindi cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya hatua zilizochukuliwa na jeshi hilo katika kudhibiti ajali na kudumisha ulinzi na usalama wa raia. Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo limeweka idadi kubwa ya askari wa usalama barabarani pamoja na askari wa kawaida katika maeneo mbalimbali ya barabara na mitaa, hivyo kuwataka madereva kuwa makini na kufuata sheria.

"Dereva yeyote atakayekiuka sheria atachukuliwa hatua haraka kwani kila sehemu wapo askari wanaohakikisha sheria zinafuatwa na kila mtu na hii pia ni kwa wale wanaokatisha safari watakiona," alisema na kuongeza:

"Vilevile wale walevi tutawaweka ndani bila hata kuwasikiliza mpaka sikukuu zishe kwani hatuwezi kuongea na mlevi tutasubiri mpaka pombe ziwaishe ndipo taratibu za kisheria zitaendelea," alisisitiza SACP Mutafungwa.

Aidha, aliwatahadharisha madereva wote ambao wamekuwa wakikiuka matakwa ya leseni zao na kuamua kuongeza nauli, kukatisha safari pamoja na kuweka magari mabovu barabarani kwa kisingizio cha sikukuu kuwa nao watadhibitiwa.

Kadhalika, aliwapongeza wananchi kwa kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo katika kipindi cha mwaka 2023 na kuwataka kuendelea kuwapa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uzembe wa madereva wanaokiuka sheria za barabarani kupitia namba yake ya mkononi pamoja na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa, Sande Ibrahimu.




Ofisa Mifumo ya Kidigitali wa Benki ya NMB, Rukia Mhendile, akichezesha droo ya kumpata mmoja wa washindi wa droo ya saba ya mastabata iliyochezeshwa katika tawi la NMB Mbagala, Dar es Salaam. Kulia ni ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Irene Kawila na katikati ni Meneja wa Tawi la NMB Mbagala, Halima Charazo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaotoa takwimu za uongo wapewa onyo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imewataka wananchi kutoa taarifa sahihi za takwimu ili kuiwezesha serikali kupanga mipango inayoendana na takwimu, kutoa msaada haraka pindi majanga yanapotokea.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, aliyasema hayo wakati wa kikao cha tano cha baraza la wafanyakazi la ofisi hiyo kilichoambatana na uzinduzi wa mkataba wa huduma kwa wateja.

Lengo la mktaba huo ni kumridhisha mteja anayetumia takwimu kutoka ofisi hiyo.

Alisema dhamira ya kutengeneza mkataba wa huduma kwa mteja ni kuongeza upatikanaji wa takwimu rasmi zenye ubora kwa ajili ya kufanya uamuzi ndani ya serikali, sekta binafsi, jumuiya za kimataifa na umma kwa ujumla.

"Kupitia mkataba huu mteja ana haki zake za msingi ambazo ni kuhudumiwa katika kiwango anachostahili, lakini kwetu sisi watoa huduma ni kuona mteja anapata huduma nzuri na kwa wakati ili kufanikisha hili tunahitaji taarifa sahihi kutoka kwa mwananchi," alisema. Alisema mkataba huo ni watatu ukichukua nafasi ya mkataba wa pili wa mwaka 2014 ambao ulitanguliwa na mkataba wa kwanza wa mwaka 2009.

Dk. Chuwa alisema katika mkataba huo NBS imeweka wazi huduma za ofisi hiyo kwa watumiaji pamoja na viwango vinavyotumika kutoa huduma ambavyo wateja watavitarajia kuvipata.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Anne Makinda alisema umoja, upendo, juhudi, maarifa na nidhamu ndiyo nyenzo ya mafanikio ya taasisi.

Hivyo, aliwataka watumishi wa ofisi hiyo kuzingatia uweledi katika utendaji kazi wao ili kutoa huduma zilizo bora na zenye manufaa kwa jamii na taifa.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, akifungua kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla alisema takwimu ni muhimu katika kutengeneza sera na mipango ya nchi.

Hivyo aliitaka NBS kuendelea kuzalisha takwimu bora ili kuchochea maendeleo.

"Tumieni vikao hivi kuzalisha takwimu sahihi kwa faida ya Taifa kwani NBS ina jukumu la msingi la kuhakikisha takwimu zinazozalishwa nchini zinakuwa bora kwa manufaa ya ufanisi wa kazi serikalini," alisema Elikana.

## Hofu ya operesheni chanzo wajawazito kujifungulia nyumbani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGANGA Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kinaga, Dk. Maria Julius, ametaja sababu nne zinazosababisha wajawazito wengi kujifungulia nyumbani mojawapo ni kuogopa upasuaji.

Sababu nyingine ni kuogopa rufani za wilaya na mkoa, elimu ya madokezo ya hatari pamoja na mazoea ya kujifungulia nyumbani yanayosababishwa na mila na desturi.

Dk. Julius alitaja sababu hizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, kwenye hafla ya uzinduzi wa kituo hicho kilichopewa jina la Ummy Mwalimu.

Alisema tabia ya wanawake kujifungulia nyumbani kunahatarishi usalama wao na watoto.

Kituo hicho kinatarajia kuondoa adha ya wajawazito kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda na kurudi katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kutafuta huduma za afya ya uzazi.

Dk. Julius alisema wajawazito wenye umri wa zaidi ya miaka 35 waliobeba ujauzito kwa mara ya kwanza, wanajifungulia nyumbani kwa kuogopa kupewa rufani ya kwenda Hospitali ya Wilaya.

Pia alitaja wajawazito waliozoea kujifungua kwa njia ya upasuaji wanakwepa kwenda hospitali au kwenye vituo vya afya wakihofu kufanyiwa upasuaji licha ya kuhudhuria kliniki zao zote.

Alisema wanawake wenye uzazi wa mimba nne na kuendelea wamekuwa wakiacha kujifungulia hospitalini kwa kile wanachokiita kuwa ni uzoefu.

"Wanaopata ujauzito kwa mara ya kwanza wanakuwa na hofu ya kujifungulia katika vituo vya afya na hospitali kutokana na elimu ya vidokezo vya hatari wanayoipata kipindi cha kliniki ya ujauzito, hivyo kuiona hatari mbele yao," alisema. Mkazi wa Kijiji cha Kinaga, John Kalugula alisema sababu nyingine inayosababisha wake zao kujifungulia njiani wakati wakielekea vituo vya afya ni kushindwa kujua makadirio yao ya siku ya kujifungua.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme alisema, lengo la serikali la kusongeza huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga vituo vya afya na zahanati ni kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi kwa wajawazito na kuwataka pindi wanapopata ujauzito waanze kliniki haraka na siyo kusubiri miezi isonge mbele.

Alisema kwa sasa kunamaradhi mengi hivyo syio vyema mjamzito kujifungulia nyumbani na kuzalishwa na mtu asiyekuwa na sifa ya ukunga au kukimbia kwa waganga wa jadi, kwamba kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha yao na vichanga vyao.

Kituo hicho kimejengwa katika Kata ya Kinaga Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kwa Sh. milioni 569.8 kati ya hizo Sh. milioni 69.8 ni mapato ya ndani ya halmashauri na Sh. milioni 500 ni fedha kutoka serikali kuu.



Ukurasa 12

Aliyebinafsishiwa kiwanda, asimulia kuegemea nishati duni kulivyokwamisha kikabaki gofu




**Panga lililokumba mashirika lihamie kwingine**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA DESEMBA 22, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Zama 'Kazi Iendelee' mtaji nishati ya REA katika makubwa ya maendeleo

## •Umeme uko vijiji 90%, safari mpya ni gesi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA ajenda ya nchi, moja ya maeneo dhahiri yanafuatiliwa kwa 'macho mawili' na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni kufanikisha umeme hasa kufika vijijini, huku akitetea mazingira kwa kuwapatia watumiaji nishati mbadala.

Hiyo inatokana na ukweli wake ni hitaji la lazima kijamii na wakati huohuo, sehemu ya ilani ya uchaguzi inayotekelezwa na awamu mbalimbali zilizopita za uongozi nchini inadai ufanikishaji wake.

Mnamo mwishoni mwa Septemba, katika hatua zake za maboresho, Rais Dk. Samia, akavunja Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kumteua Balozi Meja Jenerali Mstaafu Jacob Kingu kuwa mwenyekiti wake mpya.

Vilevile, Naibu Mtendaji Mkuu wa Serikali Msaidizi, ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, mwezi uliopita akizindua matokeo ya utafiti wa athari za upatikanaji nishati endelevu Tanzania Bara mwaka 2021/2022, ikaonyesha asilimia 72 ya kaya zote Tanzania Bara zimefikiwa na umeme.

Pia, utafiti huo ukabainisha kwamba usambazaji umeme vijijini kitaifa umefika asilimia 90. Hayo yanatokea, huku kazi hiyo imekabidhiwa wakala wa REA kuitekeleza.

Ndani ya sura hiyo kuu, kunaendana na angalizo chanya lililotewa Julai mwaka jana na aliyekuwa Waziri wa Nishati, January Makamba akitamka: "Serikali haisambazi umeme vijijini kwa ajili ya kuwasha taa peke yake, bali kuchagiza pia shughuli za kiuchumi ikiwamo uanzishaji viwanda."



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alipozindua ripoti ya nishati mwezi uliopita. **PICHA: MTANDAO**

**PICHA HALISI KINCHOJIRI**

Ni mwezi uliopita Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Biteko, akazindua matokeo ya utafiti wa Athari za Upatikanaji wa Nishati Endelevu Tanzania Bara kwa mwaka 2021/2022, unaoonyesha asilimia 72 ya kaya zote Tanzania Bara zinaishi katika vijiji na mitaa iliyofikiwa na huduma ya umeme.

Hilo liko katika utekelezaji wa kazi zake REA, sasa ikihamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, ikitamka matarajio ifikapo Julai mwaka huu, ingekuwapo mitungi 100,000 bure katika maeneo ya vijijini nchi nzima.

Hiyo ni baada ya Rais Dk. Samia kuelekeza kuwatengea shilingi bilioni 3.2 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kwa ajili ya usambazaji gesi safi ya kupikia, ufafanuzi unaotolewa na REA, ulipokutana na wadau wa gesi nchini, Mkurugenzi wa Uenezaji Masoko na Teknolojia, Mhandisi Advera Mwijage, akitamka:

"Tumefanya kikao na wasambazaji wa mitungi ya gesi na kwa hapa Tanzania sasa tuna kampuni 11 na bahati nzuri wote wamefika na ujumbe wetu kwao ni wao kuwa tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha kwamba tunasaidiana kwenye usambazaji wa nishati safi na salama maeneo ya vijijini."

Mhandisi Mwaijage akabainisha kuwa, serikali ina mipango mingi inayohakikisha wananchi wote wanafikiwa na nishati hiyo, pia wakihitaji wapate kwa wakati.

"Isiwe kama sasa ukitaka huduma ya gesi iliyojaa kuna mtu anatembea kilometa 10 hadi 30 kama mtu ana nia ya kuwa nayo kunakuwa na gharama tena ya kufuata sasa hizo ni changamoto ambazo tunatakiwa kutatua na hawa wasambazaji, ili watusaidie kusambaza huduma hizi maeneo ya vijijini ziwepo," anatamka.

Akasema, pia wataongea na wenye majiko mbadala yanayotumia gesi kidogo pia kusambaza gesi asilimia chache maeneo ya mikoa Mtwara, Lindi, na Pwani.

Ni msingi wa maoni ya awali, ambayo Dk. Biteko anaendeleza katika ripoti hiyo ya kitafiti mwezi uliopita kuhusu REA, akifafanua hadi sasa vijiji vilivyounganishwa na umeme kwa upande wa Tanzania Bara ni 11,079 sawa na asilimia 90 ya vijiji vyote (12,318).

Hapo anaendeleza kuwa, vijiji vilivyobaki 1,239 sawa na asilimia 10 vinatarajiwa kuunganishwa na umeme ifikapo Juni mwaka ujao na serikali imeshaanza kupeleka umeme katika vitongoji vyote vya Tanzania Bara katika vitongoji 15 vya kila jimbo.

Vilevile Naibu Waziri Mkuu anafafanua kuwa, serikali kupitia REA inatekeleza mradi wa kusambaza mifumo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika makazi kwenye visiwa 41 vya mikoa ya Kagera, Lindi, Mara, Mwanza na Rukwa.

Katika jukumu hilo, REA inatoa uwezeshaji wa kiufundi na kifedha, kwa waendelezaji wa miradi midogo ya nishati jadidifu katika maeneo ya vijijini, ili kuimarisha upatikanaji wa nishati umeme vijijini.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, Dk. Biteko anasema serikali inakamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia, kuhakikisha wastani asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033.

**UMEME NA GESI**

Aliyekuwa Waziri wa Nishati, January Makamba, katika ziara yake katika kiwanda kinachochakata parachichi wilayani Rungwe mkoa wa Mbeya, Julai mwaka jana, kikiwa kimeunganishwa na umeme na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), akawa na ufafanuzi wake.

Makamba akatamka ni matokeo ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali ya Rais Dk. Samia, kwamba nia ya kusambaza umeme vijijini, ni zaidi ya kuwasha

Inaendelea Uk 12

Ulivyo uja

**BIASHARA**

# Aliyebinafsishiwa kiwanda, asimulia kuegemea nishati duni kulivyomkwamisha kikabaki gofu

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

NGUVU ya serikali sasa ni kuhakikisha inapiga hatua katika kuongeza uzalishai nchini, katika nyendo tofauti za maendeleo, kwa huduma na bidhaa halisi.

Hapo ndipo anashuhudiwa mkuu wa nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anafanya ziara tofauti kimataifa kupanua soko la bidhaa nchini, pia kukaribisha nguvu za uwekezaji.

Ni katika hali hiyo, Nipashe inakutana na simulizi kinyume chake, kuanzia sera ma maelekezo kitaifa, uwekezaji unapokwama.

Mmiliki Kiwanda cha Kusindika Nanasi kilichopo kijiji cha Madeke katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Mariet Putika, ana simulizi ya mahali alikojikwaa na kuanguka kiuzalishaji.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, anaeleza sababu zilizomfanya kusitisha uwekezaji katika kiwanda hicho, ni matumizi ya nishati jua, kuni, mkaa na dizeli baada ya kukosekana nishati umeme, ambayo ilikuwa hajamfikia.

Mariet anasema, kiwanda hicho kiligharimu kiasi cha Sh. milioni 100 na kutoa ajira kwa wakazi wa eneo hilo, lakini walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nishati ya umeme, ilikwamisha ndoto yake kufanya uzalishaji.

Putika anasema, sababu ya kushindwa kuendeleza uwekezaji huo, ni kutuimia teknolojia za kizamani. Ni kiwanda alichokinunua katika mfumo wa ubinafsishaji kutoka serikalini, kupitia halmashauri hiyo kushindwa kukiendesha kwa ufanisi.

Mariet anasimulia serikali ilipompatia fursa hiyo, alifurahi sana na kuona uzalishaji wa matunda wa nanasi katika kijiji hicho ulikuwa mkubwa na akagundua kiwanda kilichopo huko hakikidhi hitaji la wananchi hao.

"Kwa kweli kile kiwanda kilikuwa kinahitaji maboresho kwa sababu kinatumia vyanzo vya aina tatu kujiendesha; kukausha nanasi, kwanza nahitaji dizeli, jua na kuni au mkaa, sasa kiwanda kimoja kinahitaji mahitaji matatu kwa wakati mmoja na kupata bidhaa iliyosawa kwa kweli ni gharama iliyo kubwa sana," anasema Putika.



Hali ya kiwanda kilichokufa katika picha tofauti Njombe. **PICHA ZOTE: ELIZABETH JOHN**

Anafafanua kwamba, kutokana na vitu hivyo vitatu kwake kuwa ni vigumu kushindwa kuendelea na usimamizi wa kiwanda hicho, kwa kuwa ilimgharimu kumfuata dizeli Njombe mjini umbali wa kilometa 130, hali iliyokuwa ngumu kuimudu.

"Ingawa kiwanda kilikuwa kimefungwa sola ili kupata nishati ya jua, lakini jua lilikuwa haliwi msimu wote, hivyo ilikuwa ni vigumu sana kufanya usindikaji wakati wote, vyote visiposhirikiana maana yake, utazalisha mananasi yasiyokauka na kubadilika rangi," anasema Putika.

Katika hilo anashauri kwamba, kwa sasa jengo hilo la kiwanda katika eneo la juu, linahitaji wataalamu walirekebishe, akifafanua: "Nilijaribu kuongea na watu wa ujenzi, wao walitoa wazo kwamba kama mimi naweza kufanya hayo matengenezo."

Anaendelea: "Maana kuna bomba pale katikati ambao linapokea maji kutoka kwenye bati na yale maji pale hayatakiwi, kwa sababu maji yakijaa linasababisha mionzi ya jua inapoingia ili ikafanye kazi ya kukausha maji yanapoteza ile nguvu ya jua."

Mwekezaji huyo anafafanua hali halisi iliyoko mahali hapo ni kwamba, panakosa kunyeshewa na mvua, vifaa vya kukausha bidhaa ikiwamo inayotoa mionzi inayotakiwa.

Pia anaeleza kutokana na changamoto hizo tangu mwanzo, uzalishaji ukashuka, akitumia mfano linganishi penye mategemeo ya kilo 20, mtu anaambulia kilo tano.

"Sasa unatoka Njombe mjini una magari, unaweka mafuta una wafanyakazi 10, unaenda kufanya kazi ya kilo tano kwa siku. Ukija kufanya hesabu hailipi, kwa hiyo pale inatakiwa matengenezo yafanyike na ikiwezekana badala ya kutumia 'draya' yenye kutaka jua, dizel, inataka kuni bora kuondoa maana haiwezi kuja kuleta faida," anasema Putika.

Mariet anaongeza kuwa, kupitia changamoto hiyo upande wa soko la kimataifa ambalo ndilo alilokuwa akilitazama zaidi, kwa uuzaji wa nanasi hizo sokoni ilikuwa ni gumu kwake kwa kuwa alikosa soko.






**MABDALA SERIKALINI**

Hata hivyo, mwishoni mwaka jana anasema serikali ilimletea mkakati wa kupunguza madhara ya matumizi ya kuni na mkaa, kwani matumizi ya mkaa na kuni yamekuwa yakitajwa kuathiri mabadiliko ya tabianchi, kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021.

"Sera inazungumzia katika yale masuala mtambuka na matatizo ambayo yapo kwenye mazingira yetu," anafafanua Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Theresia Manase.

Aidha, Nipashe, ikafika kwenye ofisi za Kituo Cha Uwekezaji TIC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kufahamu namna serikali imejipanga kuwasaidia wawekezaji wazawa wa namna hiyo, wakiwa na changamoto mbalimbali.

Ofisa Uwekezaji wa Nyanda za Juu Kusini, Privata Samson, anasema moja ya majukumu yao ni pindi mwekezaji anapojisajili kwao, wanahakikisha wanamsaidia kuwa na mazingira rafiki ya uwekezaji, kwa wote

Inaendelea Uk 14

## ZAMA 'KAZI IENDELEE' MTAJI NISHATI YA REA KATIKA MAKUBWA YA MAENDELEO

**INATOKA UK. 11**

taa, ikisonga kuchagiza shughuli za kiuchumi, ikiwamo uanzishaji viwanda.

Kwa mujibu wa Makamba, hadi Julai mwaka jana uwekezaji unaofanyika serikalini katika sekta ya nishati, umeshaongezea thamani mazao ya wakulima, akitumia mfano wa kiwanda hicho kimezalishwa ajira zaidi ya 200 kiwandani na katika mashamba ya parachichi.

Pia akafafanua msingi wa kupeleka umeme vijijini, ni kusawazisha maendeleo kati ya wakazi hao na waliopo mijini.

Meneja wa TANESCO, Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Mukhsin Kijemkuu, akamweleza Waziri wa Nishati kuwa, kiwanda hicho kabla ya kufungiwa transforma yake, kilikuwa kikizalisha lita 2000 kwa siku, lakini baada ya kupata transfoma wiki moja kikawa kinazalisha lita 4000 kwa siku.

Pia akasema gharama zake mwekezaji angetumia shilingi milioni 50 kununua dizeli ya kuendesha mitambo, ila wakati huo anatumia takriban shilingi milioni 30 kwa gharama za umeme.

Ni ziara iliyomfikisha Waziri Makamba, katika Kijiji cha Iramba, Kata ya Ntaba, wilayani humo Rungwe, kukagua kazi zinazoendelea katika chanzo cha Jotoardhicha Kiejo-Mbaka, ambacho nacho kinatarajiwa kuzalisha umeme utakaoingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Waziri Makamba baada ya kukagua chanzo hicho, akawafafanulia: "Serikali imeamua kuweka nguvu katika kuzalisha umeme kwa njia mbalimbali, tuna umeme wa maji, umeme wa gesi na safari hii tumewekeza kwenye umeme wa joto ardhi, hapa Kiejo-Mbaka. Ni moja ya vyanzo vya jotoardhi ambavyo vina uwezekano wa kuzalisha umeme wa joto ardhi."

Katika mwaka wa fedha uliopita, Wizara ya Nishati ikatenga shilingi bilioni tano kuendeleza miradi hiyo, ikinunua mtambo maalum wa kuchoronga chini kilometa tatu, kufikia joto linalotoa mvuke kuzalisha umeme.

Matarajio yaliyopo ni kupatikana umeme kiasi cha megawati 200 ifikapo mwaka 2025.

Juzi serikali ikatoa ufafanuzi upungufu wa umeme ulioko, kwamba shida itakoma ndani ya miezi minne, mradi wa umeme Mwalimu Nyerere utakapoanza kutumika.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Panga lililokumba mashirika lihamie nako kwingine






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

KUNA siku moja hivi Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, aliitisha mkutano na wahariri wa vyombo vya habari nchini, akakutana nao Dar es Salaam, akiwaambia jambo moja kubwa, kwamba ofisi yake inataka kufanya mabadiliko.

Akataja mabadiliko yenyewe yatagusa taasisi zaidi ya 300 za serikali, kwamba yatahusu ama kufuta baadhi au mengine kuyaunganisha, kwa kuzingatia utendaji na ufanisi wao katika kukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa taifa.

Hivyo, akawapa heshima na jukumu wahariri hao, kusikiliza kila taasisi kupitia vikao kazi na kuufahamisha umma, nini taasisi inafanya ili

wananchi nao wajue kama kuna umuhimu wa kubaki na taasisi zilizopo au kuziunganisha.

Kama alivyoahidi Mchechu, vikao kazi vilianza na vinaendelea katika mazingira mazuri na rafiki, huku wahariri wakipeleka ujumbe kwa umma, ili nao uone kama kuna haja ya kuendelea kuwa na taasisi hizo, katika muundo wa sasa au mabadiliko kweli yafanyike.

Sitaki kufanya tathmini ya vikao kazi hivyo na athari kwa umma, ila kueleza ni nini kinaendelea na nini kitakachofuata baada ya vikao kazi na hatua kuchukuliwa na ofisi hiyo ya Msajili, ambaye hakika ana nia njema kwa taifa hili.

Juzi kati tu hapa, wakati vikao kazi vikipamba moto, mwenye dhamana na taasisi hizo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, akaitisha mkutano na wanahabari kuelezea kinachoendelea.

Siku hiyo, akifuatana na Mchechu, Profesa Mkumbo akautangazia umma wa Watanzania, kuwa tathmini ya utendaji wa baadhi ya mashirika, umefanya baadhi yao kufutwa na mengine kuunganishwa, ili kuongeza ufanisi.

Tathmini ilibaini kuwa, baadhi ya taasisi au mashirika yanafanya kazi zinazofanana, hivyo kukosekana haja ya kuendelea kuwapo, yakiibebesha mzigo serikali hasa kutokana na kupewa ruzuku ya uendeshaji wa shughuli zao.

Mfano mdogo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inayochapisha vitambulisho vya uraia, kuungana na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), ambazo zinafanya kazi moja ya utambulisho.

Hivyo, vitaunganishwa na kuwa na shirika moja la utambulisho. Hebu fikiria nchi kuwa na Taasisi ya Utafiti wa Chai (TRIT) ya Utafiti wa Tumbaku (TORITA), ya Utafiti wa Kahawa (TACRI); au inakuwapo ya mahindi, karanga, korosho, ya magimbi, mihogo na sijui ya miwa!

Kwanini zisiunganishwe kuwa moja; ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kama ilivyofanyika sasa? Yawezekana tulichelewa sana kufikia hatua hii ambayo imetangazwa na Profesa, kwa sababu ya ama kwa kutojua au makusudi tu, ili kupeana

ulaji na ajira kwa ndugu na jamaa zetu, na kujisahaulisha kwamba ni majini yanayotunyonya damu.

Tumeambiwa hatua hii ni kama awamu ya kwanza kati ya nne ya kuchukua hatua juu ya mashirika yaliyosalia, yatakayoendelea kukutana kirafiki na wahariri na kujieleza, hivyo kutoa hatua ya tathmini kufanyika na hatimaye mabadiliko.

Wakati Watanzania tukipongeza hatua hii, tuungane kuishauri Mamlaka ya juu ya nchi, kuangalia na kwingineko ambako kuna taasisi au vyombo vinavyofanya kazi zinazofanana na ama kuziua au kuziunganisha, ikiwa ni pamoja na wizara.

Huenda hata tuna wizara nyingi na baadhi hazina tija, huku zingine zikiingiliana majukumu na hivyo kusababisha utitiri wa wizara zinazotunyonya damu kama mashirika na taasisi zilizouawa na zingine kuunganishwa?

Siyo siri, kwamba kuna wizara mizigo kama ilivyo kwa baadhi ya mawaziri, hivyo tukichanganya wingi wao na wizara, mishahara na marupurupu na matumizi mengine, tunaumba pia majini makata mengine ya kutunyonya damu.

Jiulize, Marekani ina watu zaidi ya milioni 300, lakini ina wizara 15 tu, piga ua miaka nenda rudi. Sisi tuko milioni 60, wizara zinakimbilia kuwa 30? Hapo kuna mawaziri tu, bado manaibu, makatibu wakuu, manaibu wao, na kadhalika.

Kuna wizara zinatakiwa kuuawa na zingine kuunganishwa, bila ya kuhitaji vikao kazi na wahariri, kwa sababu ni dhahiri tunaona ni wizara ipi

inafanya kazi na waziri yupi mchapakazi na nani anastahili kubaki kuwa waziri.

Mathalan, Napata tabu na kuwapo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pia ya Afya na kisha majukumu hayo nayaona ndani ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivi mnajua zote hizo zinasimamia afya au elimu? Kwanini zisiunganishwe kuwa na Wizara moja, kama kweli tunataka kubana matumizi na kuleta ufanisi?

Hii nitaifafanua siku nyingine nikigusa kila wizara, ili kuona ni jinsi gani tunabeba mzigo wa matumizi, huku tukijua tunavyoweza kulitua na kupata maendeleo, badala ya utitiri wa wizara na mawaziri? Bado bungeni, nako tutapagusa! Mungu endelea kutuweka tu!

UCHUMI

MWISHO WA MWAKA KUELEKEA 2024…

# Kampuni katika ubia na Polisi Trafiki 'Inawezekana' barabarani kuwe salama

**Na Frank Monyo**

KATIKA kuelekea kipindi cha mwisho wa mwaka, imeshuhudiwa serikali kupitia Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kikitoa tahadhari na elimu kwa madereva pamoja na watumiaji wa vyombo vya moto kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepukana na ajali za uzembe.

Ipo hoja ya kwamba ajali zinazotokea katika kipindi hiki, hasa za magari binafsi zinasababishwa na uzembe ama madereva ambao hawana uzoefu wa safari ndefu, ama kutumia vileo wawapo safarini.

Ajali za barabarani zimeacha simulizi za majonzi kwa familia za wahusika huku nyingi kati ya hizo ni tabia ya kunywa pombe na kuendesha vyombo vya moto, kundi kubwa limepoteza maisha na wengine kupata ulemavu unaotokana na ajali za barabarani.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), ajali za barabarani ni miongoni mwa sababu namba moja ya vifo kwa watoto wa umri kati ya miaka 5 hadi 14 pamoja vijana wa umri kati ya miaka 15 hadi 29 ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa.

Takwimu zinafafanua, jumla ya Watanzania 886 walipoteza maisha kati ya Januari na Novemba mwaka 2022 kutokana na ajali za barabarani wakiwamo vijana, huku wengine 573 wakiachwa na majeraha kwenye ajali 1,422 zilizorekodiwa na Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi.

Ajali hizo ziliongezeka kutoka 1,177 zilizorekodiwa kati ya kipindi cha Januari hadi Agosti 2022. Hii ina maana kuwa ndani ya miezi mitatu kulitokea ajali mpya 245.




Tukio la kuzindua kampeni ya usalama barabarani, kudhibiti ajali za mwisho wa mwaka. **PICHA: FRANK MONYO**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyowasilishwa mwezi Februari 2023 katika Bunge la 12, watu 382 wameripotiwa kupoteza maisha kutoka mwezi Oktoba hadi Desemba 2022, vifo vinavyoelezwa kuongezeka kwa asilimia 4.1 kutoka idadi ya watu 367 waliokufa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021, huku chanzo kikubwa kikitajwa ni ajali za barabarani zilizotokea katika maeneo mbalimbali nchini katika kipindi hicho.

Kutoka na hali hii, Kampuni ya Serengeti Breweries (SBL) imeanzisha 'safari ya mabadiliko' na imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kupambana na unywaji usio wa kistaarabu kupitia kampeni yake ya 'ikiwezekana'.

Juhudi hizo zinalenga kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa tabia ya kunywa kistaarabu ikisisitiza utaratibu kama ufunguo wa kuzuia maafa yanayotokana na matumizi ya kupitiliza ya pombe.

SBL inaelewa kuwa kunywa kistaarabu si tu kunasababisha usalama, afya, na ustawi kwa mtu binafsi bali pia kwa jamii kwa ujumla, kwani wananchi wote ni watumiaji wa barabara.

Hiyo ni sehemu ya kampeni hiyo, ikiwa sehemu ya uwajibikaji wa mwekezaji kwa umma au kitaalamu 'corporate social responsibility; ambayo serikali ina mwongozo wake.

Mkurugenzi wa Mahusiano ya Umma wa SBL, John Wanyacha, anasema msingi wa kunywa kwa ustaarabu uko katika uelewa kwamba jukumu la kwanza linatoka kwa mtu binafsi.

"Ni jitihada za pamoja lakini inaanza na mtu binafsi kufanya chaguo sahihi kwa ajili ya mtu binafsi, na kwa upanuzi, kwa usalama wa wengine barabarani. Kunywa kistaarabu si dhana tu; ni mazoea yanayojumuisha maisha yote. Inamaanisha kufanya chaguo linalotoa kipaumbele cha usalama, afya, na ustawi wa mtu binafsi na wale wanaotumia barabara," anasema Wanyacha na kuongeza kuwa:

"Kampeni ya inawezekana ni ushuhuda wa dhamira yetu ya kukuza tabia ya kunywa Kistaarabu ndani ya jamii yetu. Tunaamini kwa dhati kuwa kunywa Kistaarabu huanzia kwa kila mtu. Ni kuhusu kufanya chaguo sahihi kuhusu matumizi ya pombe na kuelewa matokeo makubwa ya matendo ya mtu kwenye barabara na katika jamii.

Dhana ya kunywa kistaarabu inazidi wazo la utaratibu; inasisitiza umuhimu wa kufurahia vinywaji vya pombe kwa uwajibikaji na ndani ya mipaka ya mtu binafsi. Hii inajumuisha kuelewa uvumilivu wa mtu, kujua wakati wa kutokunywa, na muhimu zaidi, kutokunywa na kuendesha gari."

Anasema kampeni hiyo inalenga kushughulikia matumizi mabaya ya pombe hasa katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Wanyacha, anasema kuwa mustakabali wa SBL ni kung'aa katika kuhakikisha usalama watanzania wote, kwa kutoa elimu na kuhamashisha matumizi ya pombe kistaarabu. "SBL kupitia kampeni hii inatumia majukwaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na programu za elimu, jitihada za kukuza uelewa, na ushiriki wa jamii, kufikia kila kona ya nchi. Inawezekana inajitahidi kuwaelimisha umma kuhusu hatari za kunywa na kuendesha gari pamoja na hayo, umuhimu wa kunywa kwa uangalifu," anasema.

# Aliyebinafsishiwa kiwanda, asimulia kuegemea nishati duni kulivyokwamisha kikabaki gofu

Inatoka Uk 12

wazawa na wageni.

"Mwekezaji ambaye amejisajili kwetu na akasitisha uwekezaji anatakiwa kututaarifu sisi kwamba nimekutana na changamoto moja, mbili, tatu ndiyo maana nimesitisha uwekezaji, ili sisi kama kituo tuone tunamsaidiaje. Kwa hiyo jukumu letu sisi ni kuhakikisha hakutani na vikwazo," anasema Saimon.

Anabainisha kwamba, ukanda huo wenye mikoa saba ikiwamo Njombe, hadi kufikia Oktoba 2023, wamefanikiwa kusajili miradi 646, inayotarajia kutengeneza ajira zaidi ya 100,000.

"Miradi hiyo inategemea kuleta mtaji wa dola za Kimarekani na Sh. milioni 248,334 kwa aina ya mkoa wenyewe ulivyo na sekta ambayo inaongoza. Kwa kusajili miradi, ni sekta ya 'manufacturing' (uzalishaji) utengenezaji), sekta inayofuata ni kilimo na sekta nyingine ambazo hazijapishana pishana sana," anasema.

Simon anasema, mkoa wa Iringa unaongoza kuwa na miradi 229, ukifuatiwa na Mbeya miradi 222, Ruvuma 56, Njombe na Rukwa miradi 53.

"Kigezo cha kwanza ili usajiliwe na TIC, ni lazima uwe na kampuni kwa sheria ya zamani, sheria ya sasa hivi inaruhusu mtu binafsi asajili ila ya zamani ambayo tulitumia mpaka mwaka jana ilikuwa lazima uwe na kampuni," anasema.

Simon anaeleza kuwa uwekezaji una faida nyingi kitaifa zikiwamo kutengeneza ajira, kuleta fedha za kigeni, kupatia nchio kodi, kukuza uchumi na kubadilisha hadhi ya taifa kukua zaidi.

Anasema, faida ya mwekezaji kujisajili TIC ni pamoja na kutatua changamoto ambazo wanakutana nazo wawekezaji, huku Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 imebainisha malengo mahsusi sita na malengo nane ya kisekta.

Baadhi ya malengo hayo, anayataja ni kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje, kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi, kuhimiza na kuvutia matumizi ya teknolojia za kisasa katika uwekezaji,kuweka mfumo mzuri na wa wazi wa kisheria na kuondoa urasimu katika taratibu za upatikanaji wa vibali vya uwekezaji.

# Mchengerwa akabidhi 'ambulance' 5, atoa angalizo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amekabidhi magari matano kwa Mkoa wa Dodoma yatakayotumika kwenye shughuli za huduma za afya.

Hafla ya kukabidhi magari hayo ilifanyika juzi kwenye viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma.

Akikabidhi magari hayo Mchengerwa aliwataka waganga wa halmashauri za Mkoa wa Dodoma kuyatumia kwa uadilifu kama ilivyokusudiwa ili kuwasaidia wananchi. "Mheshimiwa Rais amezitoa gari hizi tano kwa Watanzania, mpango wa serikali ni kila halmashauri kupokea gari moja na kila jimbo la uchaguzi lipate gari ya kubebea wagonjwa," alisema. Aidha, alisema hadi sasa Dodoma imepokea gari tatu kwenye halmashauri za Mpwapwa, Chamwino na Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe.

Alisema takribani Sh. bilioni 52 zimetolewa kununua gari 528 kati ya hizo 316 ni gari za kubebea wagonjwa na nyingine 212 kwa ajili ya kutumika na waganga wa mikoa na wilaya," alisisitiza Mchengerwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa gari hizo kwa mkoa wake kwani zitasaidia kurahisisha utoaji wa huduma za afya.

"Gari hizi zitawezesha usimamizi wa shughuli za miradi ya afya sambamba na kutoa huduma tembezi ndani ya mkoa kwani serikali imekua ikitoa fedha nyingi kwenye sekta ya afya, hivyo tunaahidi kutunza gari hizi na kuzitumia kama ilivyokusudiwa," alisema. Alisema Mkoa wa Dodoma unahitaji gari 79 za kubebea wagonjwa ambapo mpaka sasa wameshapata gari hizo kwa asilimia 34.



Wafanyakazi wa Shirika lisilo la kiserikali la Trees for the Future Tanzania kutoka mikoa ya Singida, Tabora, Iringa na Simiyu wakikagua kitalu cha mboga na miti jana kwa mnufaika, Issa Chufa, mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, walipoenda kujifunza jinsi wanufaika wanavyotekeleza miradi inayofadhiliwa na shirika hilo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Polisi, LATRA wafanya operesheni ukaguzi magari mabovu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) limeanzisha operesheni maalum ya kukagua mabasi na madereva walevi.

Lengo kuu ni kudhibiti ajali ambazo zimekuwa zikitokea kipindi cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumza wakati akiongoza operesheni hiyo iliyofanyika katika Kituo Kikuu cha Mabasi Misuna, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Stella Mutahibirwa, alisema operesheni hiyo wanayoifanya inalenga kuhakikisha magari yote yanayoingia Mkoa wa Singida yanaingia na kutoka yakiwa salama.

Alisema LATRA na Jeshi la Polisi wanaendelea kutoa elimu kwa madereva, makondakta wa mabasi na abiria ili wanapoona dereva anaendesha mwendokasi ambao unahatarisha usalama wao waweze kutoa taarifa.

Alisema katika operesheni hiyo wamebaini kuwa mabasi mengi hayana mikanda ya usalama na iliyopo ni mibovu, kwamba tatizo lingine ni wazazi wanaposafiri na watoto wao zaidi ya wawili kutowakatia tiketi za siti zao jambo ambalo sio nzuri kiusalama.

Alisema madereva wanapoingia katika kituo hicho cha mabasi huwapima kama wamekunywa pombe kwa kutumia kifaa maalumu na kutoa elimu kwa abiria kuwa wanaposafiri na kuona dereva anakwenda mwendo wa kasi watoe taarifa kwa Jeshi la Polisi kupitia namba za wakuu wa jeshi hilo zilizopo kwenye mabasi hayo.

"Sisi Jeshi la Polisi jukumu letu ni kulinda maisha ya raia na mali zao, hivyo tumeamua kufanya operesheni hii ya kutoa elimu kwa abiria ili waweze kujua haki zao na kutoa taarifa pale wanapoona madereva wakiendesha mwendo kasi," alisema.

Alisema wamezungumza na abiria na madereva kuhusu wajibu wao wanapokuwa wanaendesha magari na kuwataka kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa za usalama barabarani na kuhakikisha wanawafikisha abiria wao salama wanakokwenda na kuwa kauli mbiu yao ya mwaka huu inasema 'ukimya wako ni umauti wako paza sauti.

Aidha, Kamanda Mutahibirwa alisema abiria nao wanajukumu la kulisaidia Jeshi la Polisi kukemea maovu yanayofanyika pindi wanapokuwa kwenye safari yakiwamo ya mwendo kasi na dereva anayeyapita magari mengine kwa wakati mmoja na eneo ambalo sio sahihi.

Hivyo, aliwataka abiria wakati wote wanaposafiri kujenga tabia ya kufunga mikanda ambayo imewekwa mahususi kuwasaidia pale gari husika litakapopata changamoto ya dereva wake kusisima kwa ghafla au kupata ajali.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mkoa wa Singida, Layla Dafa, alisema wamekuwa wakiyakagua mabasi hayo ili kubaini makosa mbalimbali ambayo yanafanywa na madereva na makondakta.

Alisema moja ya makosa hayo ni kutowakatia abiria tiketi za kielektroniki ambapo wamewasisitizia sana abiria kutumia tiketi hizo ili wasizidishiwe nauli wanaposafiri.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mawakala wa Mabasi Stendi Kuu ya Misuna, Msafiri Ndui alisema wakati wote unapofika msimu wa abiria wengi baadhi ya mawakala wasiowaaminifu wamekuwa wakipandisha bei ya nauli.

# Wakaguzi mbolea wapewa mafunzo kuongeza ufanisi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imewataka wakaguzi waliohitimu mafunzo ya ukaguzi kutumia mafunzo yao kwa vitendo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Pia, wametakiwa kutojihusisha na vitendo vya rushwa, badala yake wakafanye kazi waliokabidhiwa ya kuwahudumia wakulima.

Meneja Uhusiano, Mawasiliano na Elimu wa TFRA, Matrida Kasanga, alitoa maelekezo hayo juzi wakati wa mafunzo hayo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Matrida alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kufanya ukaguzi kwa kuzingatia ubora wa mbolea na usimamizi wa mfumo wa ruzuku.

Alisema washiriki hao kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, wamejifunza sheria, kanuni na taratibu ambazo zitatumika katika tasnia ya mbolea.

Alisema ni matarajio yao kuwa watendaji watatenda haki katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo kutoa elimu kwa wakulima ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku.

Alisema mafunzo ya siku tatu ambayo washiriki yakawe chachu kwao ya kufanya kazi kwa bidii, huku wakikumbuka kile walichofundishwa kwa vitendo.

Alisema wakaguzi ni watu wa muhimu katika jamii, hivyo wakafanye kazi waliotumwa na serikali na siyo kukiuka maadili ambayo wamekula kiapo kabla ya kuanza utendaji wao.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya rushwa kwa wakaguzi hao, aliwataka kuepukana na vitendo hivyo badala yake wakafanye kazi kwa weredi walioagizwa na serikali. Alisema vitendo vya rushwa vinapotosha uadilifu kwa watendaji huku akiwasisitiza kuacha tamaa ya pesa badala yake wafanye kazi kwa bidii.

Mshauri wa kilimo Mkoa wa Morogoro, Dk. Rozalia alisema wakaguzi hao watapewa mwongozo udhibiti ubora wenye lengo la kuwa na wakaguzi bora ambao wataleta matokeo chanya.

Alisema anaamini mafunzo hayo yamewapa uwezo wa kubaini mbolea ambazo zimepungua ubora na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika watakaobainika na changamoto hizo.

Alisema Tanzania imekuwa ikitumia kati ya tani 300,000 hadi 600,000 za aina ya mbolea mbalimbali kwa mwaka, ambapo ni sawa na asilimia 30 hadi 60 ya lengo ambalo ni sawa na tani milioni moja.





# CCM Njombe yakemea tabia watoto kwenda 'disko'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe kimeiagiza serikali kupiga marufuku wanawake wenye watoto wadogo mkoani Njombe kwenda sehemu za starehe na kunywa pombe kama njia moja wapo ya kukabiliana na udumavu na utapiamlo.

Agizo hilo limetolewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa Njombe, Daniel Okoka, wakati akizungumza na wananchi baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa ilani katika Kata ya Majengo iliyoko Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe.

Alisema ni jambo ambalo halikubaliki kuona mama mwenye mtoto mdogo anashinda baa au kwenye vilabu vya pombe wakati mtoto wake anasumbuliwa na udumavu.

Pia alimwagiza Mtendaji wa Kata ya Majengo kuwakamata wazazi wanaoshinda baa na kwenye vilabu kunywa pombe wakati watoto wao wamepimwa na kuonekana hali zao ni mbaya zaidi katika udumavu.

"Akae nyumbani atunze mtoto wake mpaka pale afya itakapoimarika ndiyo mwambie njoo kilabuni unywe bia vinginevyo tutapoteza watoto hawa," alisema Okoka.

Alisema wapo kinababa ambao wanadhani jukumu la kulea ni la wanawake pekee na kushindwa kuwajibika wanatakiwa kufuatiliwa ili hatua za makusudi ziweze kuchukuliwa.

Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji wa Makambako, Dk. Ally Senga alisema suala la udumavu ni changamoto kubwa kwenye mikoa ya kusini ambapo Mkoa wa Iringa unaongoza na kufuatiwa na Njombe yenye asilimia 50.4 ya udumavu.

Alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha changamoto kubwa ya watoto kuwa na udumavu ni ulaji duni na watu kushika mimba katika umri mdogo.

Alisema halmashauri hiyo iliwapima watoto 597 lakini kati yao 148 walionekana kuwa na udumavu lakini Kata ya Majengo katika watoto 59 waliopimwa 17 pekee walikutwa na udumavu.

Mkazi wa Kata ya Majengo Mjini Makambako, Oliver Abely alisema kwa sasa asilimia kubwa ya wanaohangaika kwenye familia katika kutafuta mahitaji ya nyumbani ni wanawake hivyo wanakosa muda wa kuwapikia watoto vyakula ambavyo vinazingatia mlo kamili.

# ...Yatoa mbegu za korosho kwa serikali mkoani Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetoa kilo 400 za mbegu za korosho kwa Serikali ya Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuwapatia bure wananchi wa maeneo ambayo zao hilo linastawi.

Mbegu hizo zilikabidhiwa juzi na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi yake kwa wananchi wa mkoa huo ya kufufua baadhi ya mazao ya biashara.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mbegu hizo, Mwalunenge alisema mbegu hizo zilikabidhiwa kwa chama hicho na uongozi wa Bodi ya Korosho Tanzania ambayo ndiyo inayosimamia zao hilo.

Alisema chama hicho kiliomba mbegu hizo kama sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya chama taifa ya kuhakikisha wananchi wanainuliwa kiuchumi kwa kuwaboreshea mazingira ya uzalishaji wa mazao mbalimbali.

"Sekta ya kilimo inaajiri karibia asilimia 80 ya Watanzania wote kwa hiyo sisi kama chama tunahakikisha kwamba tunaboresha njia zote za uzalishaji kwenye sekta hiyo, hapa leo tunaanza na korosho lakini na mazao mengine tutafuata," alisema Mwalunenge.

Aliyataja mazao mengine ambayo wanakusudia kuwasaidia wakulima kuwa ni kahawa, kakao, pareto na mazao mengine ya biashara ambayo itabainika kuwa yanastawi mkoani humo.

Mwakilishi wa Bodi ya Korosho nchini, Mandela Chikawe, alisema mbegu hizo zilizokabidhiwa zikioteshwa vizuri zina uwezo wa kuzalisha miche 56,000 ambayo ikipandwa kwa kufuata taratibu zote inatosha kwenye mashamba yenye ukubwa wa ekari 2,000.

Alisema mbegu hizo ni sehemu tu ya mkakati wa bodi hiyo na kwamba wataendelea kupeleka zingine wakishirikiana na serikali ya mkoa ili wananchi wengi zaidi waendelee kulima.

Alisema mbali na kugawa mbegu hizo pia wanakusudia kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mbeya kwenye utaalamu wa uzalishaji wa miche hiyo pamoja na taratibu za kupanda ili wananchi wawe na uelewa wa kutosha.

"Korosho ni miongoni mwa mazao ya kimkakati kwa hiyo hizi mbegu ni za kuanzia lakini tutaendelea kuleta zingine ili maeneo yote ambayo yamebainika kuwa zao hili linaweza likastawi wananchi wapande," alisema Chikawe.

Mwakilishi wa wakulima, Felix Lyaniva alisema korosho ni miongoni mwa mazao ambayo yanaweza yakatumikwa kama pensheni kwa wastaafu kutokana na kwamba ni miongoni mwa mazao ambayo yanavunwa muda mrefu.

Hivyo, aliwasihi wakulima wa maeneo mbalimbali ya mkoa huo ambayo yamebainika kuwa zao hilo linastawi kuchangamkia fursa hiyo ili kujiwekea mazingira mazuri ya uchumi.

Akipokea kwa niaba ya Serikali ya Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema watagawa mbegu hizo kulingana na ukubwa wa maeneo ya uzalishaji kama ambavyo utafiti umefanyika.

Alisema atawasiliana na wakuu wa wilaya zote za mkoa huo ili kukubaliana namna ya kuzigawa kulingana na maelekezo ya viongozi wa CCM mkoa.



Wafanyakazi wa Shule ya Sekondari ya Patrick Mission Dar es Salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya wakigawa misaada ya vyakula kwa wazee wasiojiweza katika Kata ya Santiliya, wilayani Mbeya juzi kwa ajili ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, zaidi ya 300 wamenufaika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanandoa 61 wawasilisha maombi kudai talaka Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANDOA 61 wamepeleka maombi ya kudai talaka katika Baraza la Kata Kivavi Mjini Makambako Wilaya ya Njombe kwa kipindi cha kuanzia Novemba hadi Desemba 20 mwaka huu.

Mwenyekiti wa Baraza la Kata Kivavi, Muhimba Payovela, alisema hivi sasa anapokea migogoro mingi ya wanandoa kuliko ile ya ardhi.

Mwenyekiti huyo, alisema sababu kubwa ya wanandoa wengi kudaiana talaka ni kutoaminiana miongoni mwao na wengine kuendekeza tamaa.

"Kuharibika kwa familia kuna athari kubwa sana kwa sababu watoto watabaki bila ya matunzo, watoto watakosa huduma za baba na mama na ukizingatia ndoa inapovunjika watoto wanabaki peke yao na wababa wachache sana wanaomudu kulea watoto," alisema Payovela.

Aidha, Payovela alisema baada ya wanandoa kupeana talaka wanaume wengi wameshindwa kutekeleza wajibu wao wa kimalezi kwa watoto wao.

Baadhi ya wanaume na wanawake Mjini Makambako walisema migogoro mingi ya ndoa inachangiwa na wengi wao kutoridhika na walichonacho na baadhi ya wanawake kutaka usawa ndani ya ndoa zao, huku wengine ikiwa ni vitendo vya ukatili wanavyokutana navyo.

"Wanawake wengi siku hizi wanataka usawa katika ndoa, ujue mimi ni mwanaume siwezi kukubali kila kitu unachokitaka wewe nikubali hiyo hapana," alisema Jovin Mlelwa.

Nao viongozi wa kidini akiwamo Shekhe wa Msikiti wa Masjid Sulemani Ubena, Muharami Nyalusi na Mchungaji wa Kanisa la The Tabanacle Assembles of God, Charles Mwidete walisema migogoro ya ndoa inaongezeka kutokana na wanandoa kukosa uadilifu na kukosa elimu ya ndoa.



## ZAWA yaagizwa kusimamia mradi pampu za umeme jua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, ameitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuhakikisha inasimamia mradi wa uwekaji wa pampu za maji zinazotumia umeme wa jua katika visima vya maji ili kuzalisha maji kwa gharama nafuu.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Mjini Zanzibar, katika hafla ya utiaji saini wa ushirikiano kwa kampuni ya Scan Investment ya Oman kwa mradi wa uwekaji wa Solar Pump za visima vya maji.

Alisema serikali inatarajia kupata mafanikio makubwa hususani katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji nchini.

Alisema Zanzibar inauwekezaji mkubwa, hivyo ni vyema wakaharakisha kufikia malengo ambayo yamewekwa na wananchi wanategemea kunufaika kupata majisafi na salama.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza gharama za matumizi ya umeme katika visima vya maji.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji (ZAWA), Dk. Salha Kassim Muhammed, alisema visima 79 vitawekewa huduma ya pampu za umeme wa jua.

Alisema, huduma hiyo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza uendeshaji wa kupandisha na kusambaza maji katika maeneo yote yaliyolengwa.

Pia alisema mradi huo utalenga zaidi katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa kusambazwa awamu kwa awamu hadi kukamilika kwake.

Alisema kuwa awali kampuni hiyo pamoja na wataalamu wazawa walifanya utafiti kwa kuviangalia visima vyote vya mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema zoezi hilo likikamilika wanatarajia kusambaza huduma hiyo kwa mikoa mengine, baada ya kujiridhisha kuwa solar hizo zinafanya kazi vizuri na kusaidia kuzalisha maji ili kutoa huduma kwa wananchi.

# Vyuo vikuu vyapewa siri ya kupata maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, amesema kuanzishwa kwa mkusanyiko wa kitaaluma na vyuo vikuu ni kichocheo cha mabadiliko na ustawi wa chuo katika utendaji na kuchangia kasi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya mkusanyiko wa kwanza wa kitaaluma na utoaji wa tunzo kwa waanzilishi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), iliyofanyika Maruhubi visiwani hapa, ikiwa ni miongoni mwa maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Waziri huyo alisema hivi sasa dunia inawatumia wasomi, wahitimu katika kufanikisha utayarishaji na utengenezaji wa sera na mipango ya kimaendeleo ya nchi.

Alisema ni matumaini yake kwamba mikusanyiko hiyo ya kitaaluma kwa waliopita kwenye mikono ya SUZA wataitumia fursa hiyo kwa kuleta mabadiliko chanya.

Aidha, aliwataka wanataaluma hao, watumie uwezo wao kukishauri chuo kwa mambo mazuri yatakayokiwezesha kutoa wahitimu bora, watakaoleta ushindani kwenye soka la ajira na kuwa na uwezo wa kujiajiri.

Hivyo aliwataka waandaaji wa mkusanyiko huo kutorudi nyuma na wakubali kujifunza kwa wenzao ambao wamefanikiwa kupitia mikusanyiko hiyo na kuwataka kuzingatia muda na wakati kwa kila shughuli wanayojipangia.

Akizungumzia kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar, alisema wanakila sababu ya kusherehekea na kujivunia, kutokana na matunda waliyonayo ambayo yanatokana na mapinduzi yao tangu mwaka 1964. Alisema mijadala hiyo itatoa fursa kwa wanataaluma, viongozi wa sasa na wajao kuona namna gani wanatafsiri katika utendaji wa shughuli zao za kila siku na katika kuhakikisha nchi yao inafikia dhamira ya kupiga hatua kimaendeleo.

Naye Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Mohamed Makame Haji, alisema wazo la kuanzishwa kwa chuo hicho ambacho sasa kinatimia miaka 21 lilitolewa na baadhi ya watu ambao kama chuo wameona kuna haja ya kuwatunukia tunzo ili mchango wao kutambulika.

Alisema uongozi wa chuo hicho utaendelea kushirikiana na Rais wa Zanzibar ambaye ndiye mkuu wa chuo hicho kwa kutoa elimu bora ili kuwa sehemu ya vyuo vikuu bora nchini.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa chuo, Dk. Ali Makame Ussi, alisema miongoni mwa mafanikio ya chuo ni kuwa na uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya jamii na taifa, kwamba chuo kinajivunia kuwa na wahitimu wengi katika fani mbalimbali ambapo wanatoa huduma na kusaidia jamii.

Alisema mkusanyiko huo wa kitaaluma ni sehemu ya jitihada za kupanua wigo na kuongeza ukubwa wa chuo hicho, kimetoa wahitimu wengi tangu kilipoanzishwa miaka 20, imetoa wahitimu 15,866 zaidi ya 9,000 ni wanawake na zaidi ya 6,000 ni wanaume.

Alisema hiyo ni fursa ya kujivunia katika kuelekea miaka 60 ya mapinduzi na kuleta ufanisi ili kufikia malengo yaliokusudiwa.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kushoto), akiwa katika maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kuelezea mafanikio ya wizara yake kwa kipindi hicho mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matukio 172 ya ukatili, udhalilishaji yaripotiwa Novemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MATUKIO 172 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika kipindi cha Novemba 2023, ambapo waathirika wengi wakiwa ni watoto.

Mtakwimu kutoka Divisheni ya Jinsia na Ajira katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Ramla Hassana Pandu, alitoa takwimu hizo na kusema idadi hiyo kwa Novemba yamepungua kwa asilimia 13.6 kutoka matukio 199 yaliyoripotiwa Oktoba 2023.

Ramla alisema idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 2.8 kwa kuripotiwa matukio 172 kwa kipindi cha Novemba 2023 ikilinganishwa na matukio 177 yaliripotiwa Novemba 2022. "Kwa Novemba 2023, idadi za makosa ya ukatili na udhalilishaji ni makosa ya shambulio la aibu au kukashifu yalikuwa 18, makosa ya shambulio 32, kubaka 80, kulawiti na kunajisi 21, kuingilia kinyume na maumbile 11 na kutorosha makosa 10," alisema.

Akizitaja wilaya zinazoongoza kwa matukio ya ukatili na udhalilishaji ni Wilaya ya Mjini na Wilaya Magharibi 'B' Unguja zimeripotiwa kuwa na matukio mengi zikilinganishwa na wilaya nyingine.

Alisema Wilaya ya Magharibi B imeripotiwa kuwa na matukio 47 sawa na asilimia 27.3 na Wilaya ya Mjini yameripotiwa matukio 42 sawa na asilimi 24.4, Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio mawili sawa na asilimia 1.2 ikilinganishwa na wilaya zingine.

Aidha alisema Wilaya ya Magharibi B imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya kubaka ikilinganishwa na wilaya nyingine kwa matukio 22 sawa na asilimia 27.5 kati ya matukio yote ya kubaka yaliyoripotiwa.

"Kati ya matukio 80 ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Novemba 2023, matukio 8 sawa na asilimia 10.0 yameripotiwa kwa wanawake na matukio 72 yameripotiwa kwa wasichana sawa na asilimia 90.0," alisema.

Akitaja hatua zilizochukuliwa alisema kuwa kati ya matukio yote 172, matukio 122 yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 70.9, matukio 49 sawa asilimia 28.5 yapo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na tukio moja sawa na asilimia 0.6 lipo mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHAFII RAMADHANI MSUYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 803 DJZ – NISSAN CARAVAN.** Chassis namba **ARE24032627.** Engine namba **TD2EAA2627.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/9651/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MASEKE JUMA MARWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 615 DQP – TOYOTA CROWN.** Chassis namba **GR1805006281.** Engine namba **4GR0018354.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/3597/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOEL ERINEST NDOSSI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari , yenye namba za usajili **T 231 AUY Toyota Staut** Chassis Namba **YK1100003774,** Engine Namba **4Y022068.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **PHQ/KIL/SAM/6400/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILIAN BLANDINA NAMBEYE** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili, **T382CVQ,** ENGINE NO. **QG15450192.** CHASSIS NO. **FG10006573.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/ARU/ARU/9739/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHICHI KARIMA MHANDENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 649 CAV – TOYOTA HARRIER.** Chassis namba **MCV100002148.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/57962/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IVORY TOWER LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 660 DEY – TOYOTA.** Chassis namba **JTEGH23B900018881.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/57809/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM ALIBARIK JONATHAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 426 CKM – SUZUKI CARY.** Chassis namba **DC511227877.** Engine namba **F6A900835.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/57069/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI Kituo Cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 101 /2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DAMARY. M. KUSENHA WA KIGAMBONI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA BARAKA JOB KUSSENHA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Wafanyakazi wa Tume ya uchaguzi na mawakala wa vyama wakiendelea kuhesabu kura katika moja ya kituo cha uchaguzi nchini DRC

# Vurugu zatawala uchaguzi DRC

## •Vituo vyachomwa moto, wagombea wataka urudiwe

**KINSHASA, DRC**

WASIWASI watanda nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya zoezi la upigaji kura uliodumu kwa siku mbili kugubikwa na vitendo vya ghasia, ikiwamo baadhi ya vituo kuchomwa moto na wananchi wenye hasira.

Uchaguzi huo uliofanyika Jumatano, ulikumbwa na ucheleweshaji wa vifaa katika maeneo mengi na kuibua madai ya kuwepo kwa udanganyifu wa kura.

Baadhi ya vituo ambavyo havikufanya kazi Jumatano kutokana na kukosa vifaa, zoezi la upigaji kura liliendelea jana lakini baadhi ya maeneo yalikumbwa na ghasia.

Wagombea wanne wa upinzani wamemtuhumu Rais Filex Tshisekedi kuharibu uchaguzi kwa makusudi na kutoa wito wa kufutwa na kurudiwa upya.

Rais Tshisekedi ambaye anawania muhula wa pili, anakabiliwa na upinzani kutoka wagombea 18.

Watu milioni 44 walijiandikisha katika daftari la wapigakura.

DRC yenye eneo mara nne kwa ukubwa na nchi ya Ufaransa, haina miundombinu ya kutosha na kusababisha miji yake mikubwa kutounganishwa na barabara.

Katika kusaidia usambazaji wa vifaa katika maeneo ya vijijini, Umoja wa Mataifa ukishirikiana na nchi za Misri na Congo-Brazzaville zilisaidia kusafirisha kwa kutumia helikopta na ndege zingine ndogo.

### KURA ZAHESABIWA

Pamoja na kuwapo kwa malalamiko hayo, Tume ya Uchaguzi nchini humo (CENI) imeanza kazi ya kuhesabu kura kwa vituo vilivyokamilisha zoezi la upigaji kura.

Katika baadhi ya vituo, watu waliendelea kupiga kura zao hadi za jana asubuhi kutokana na kuwapo kwa changamoto kadhaa za vifaa.

Mkuu wa kituo kimoja cha kupiga kura Marie Ufaransa, alisema baadhi ya vifaa vya kielektroniki vilivyoharibika siku ya kwanza vilibadilishwa baada ya kuchelewa, ukosefu wa umeme na matatizo mengine.

Alisema vituo vyote vilifunguliwa jana na kufungwa baada ya kukamilisha kazi hiyo.

Jumla ya vituo vya kupia kura 75,000 vilikumbwa na matatizo kati ya 175,000 vilivyopaswa kuwahudumia watu milioni 43.8 wenye sifa za kupiga kura.

### VITUO VILICHELEWA

Licha ya uratibu kuwa wa kusuasua, baadhi ya vituo katika Jiji la Kinshasa vilichelewa kufunguliwa na kusababisha kuibuka kwa vurugu kutoka kwa watu waliowahi kufika asubuhi kupandwa na hasira.

Mwanamke mmoja katika mji wa Kinshasa aliiambia BBC kuwa alilazimika kupigana akiwa ndani ya kituo ili kupata nafasi ya kupiga kura.

"Kulikuwa kama machafuko, nilikanyagwa chini ya miguu." Alisema mwanamke huyo.

Mpigakura mwingine alisema alirudi nyumbani baada ya kushindwa kupiga kura kufuatia kituo alichotakiwa kutimiza haki yake kufungwa kwa kukosa nishati ya umeme.

Mgombea urais kutoka chama cha upinzani, Martin Fayulu, alikaririwa akisema kwamba uchaguzi huo ni sawa na machafuko kamili. Shirika la habari la Reuters liliripoti kwamba mgombea mwingine wa urais, Denis Mukwege, alidai uchaguzi huo ni udanganyifu wa karne. Fayulu, Mukwege na wenzao wawili waliungana na kutoa wito wa kurudia uchaguzi huo.

Mfanyabiashara Milionea Moïse Katumbi alisema ni mapema sana kutoa kauli, lakini alikiri kulikuwa na mapungufu mengi.

Kulingana na kundi la waangalizi la Symocel, walitoa tathmini yao kuwa karibu asilimia 60 ya vituo vya kupigia kura vilichelewa kufunguliwa, huku asilimia 30 za mashine za wapigakura zilikuwa na kasoro.

Mkuu wa uchaguzi wa taasisi hiyo, Denis Kadima, alisema kulikuwa na majaribio 3,244 ya kudukua mifumo ya kompyuta ya taasisi hiyo.

Alisema katika mji wa kaskazini-mashariki wa Bunia, watu hawakuweza kurejea katika vijiji vyao vya kupiga kura, walishambulia na kuchoma moto kituo kimoja na kusababisha mashine na karatasi za kura kuteketea.



Kundi la wapiga kura nchini DRC walioshindwa kutimiza haki yao baada ya kituo kushindwa kufunguliwa kutokana na matatizo ya umeme juzi

### OMBA

Aidha, kuna baadhi ya maeneo hakukufanyika upigaji kura kutokana na kukumbwa na uasi kutoka kwa vikundi mbalimbali vyenye silaha.

Kwa mara ya kwanza, raia wa DRC wanaoishi katika nchi tano ikiwamo Afrika Kusini na Ubelgiji walipiga kura.

### DOSARI DAFTARI

Matatizo mengi yalijitokeza pale wapigakura walipokosa kuona majina yao kwenye daftari la kupigia kura.

Katika Jiji la Kinshasa vituo vya kupigia kura vilikuwa havijafungwa hadi saa tano usiku na kuibua wasiwasi kwa wafuasi wa vyama vya upinzani.

Hata hivyo, Tume ya Uchaguzi inalaumiwa kwa kushindwa kusimamia uchaguzi huo licha ya kutumia dola bilioni 1.2 kufanya maandalizi.

Katika Mji wa Goma, vituo kadhaa vya kupigia kura vilifunguliwa saa sita mchana na kusababisha watu wenye hasira kuvamia vituo hivyo na kisha kuviharibu kwa kuchoma moto.

Kulikuwa na mkanganyiko pia katika eneo la Kanyarucunya baada ya majina ya watu waliohamishwa kuchanganywa na yale ya wenyeji kwenye orodha ya wapigakura yalibandikwa kwenye vituo.

### CHAMA CHA KABILA

Chama cha Common Front for Congo (FCC) kilitoa taarifa yake na kueleza kwamba uchaguzi mkuu waliuvuruga. Taarifa ya chama hicho kinachoongozwa na rais wa zamani, Joseph Kabila, kilisema Rais Tshisekedi na Tume ya Uchaguzi walipanga na kuhusika na vurugu hizo.

### KAULI YA WAANGALIZI

Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi huo (CENCO-ECC) umetoa ripoti yake ya awali kuhusu uchaguzi huo na kueleza asilimia 31.37 ya vituo vya vyote vya kupigia kura havijafunguliwa siku ya kwanza na asilimia 45.1 vilipata hitilafu ya vifaa vya Kielektroniki vya kupigia kura.

Aidha, asilimia 9.8 ya vituo vya kupigia kura waangalizi hawakuruhusiwa kwenda, huku asilimia 7.84 ya vituo hivyo viliripotiwa kuwapo kwa vurugu ikiwa pamoja na kuharibiwa.

Ripoti hiyo iliendelea kusema kuwa mvua ilitatiza shughuli ya upigaji kura kwa asilimia 3.92.

Waangalizi hao wa CENCO-ECC MOE, walisema ripoti hiyo inatokana na takwimu zilizopokelewa kutoka asilimia 22.1 ya waangalizi wake waliokuwa katika maeneo mbalimbali nchini humo.

Ujumbe huu wa waangalizi, uliitaka CENI kutoa ufafanuzi kuhusu vituo ambavyo havikufunguliwa na vile ambavyo vilichelewa kufunguliwa, kwa lengo la kuheshimu ibara ya 52 ya sheria ya uchaguzi ya nchi hiyo.

Pia ujumbe huo ulipendekeza serikali, kuhakikisha uwepo wa usalama wa raia, mawakala wa CENI na vifaa vya uchaguzi kwenye vituo vya kupigia kura.

### MSHINDI ATAPATIKANA VIPI?

Kama mgombea wa kiti cha urais atashindwa kuvuka asilimia 50 ya kura zote, utaitishwa uchaguzi wa duru ya pili na kuwashindanisha wagombea wawili waliopata kura nyingi.

Kutokana na uchaguzi huo kuwa na idadi kubwa ya wagombea wa nafasi hiyo, Rais Tshisekedi anaweza kunufaika kwa kupata asilimia zaidi ya 50 inayotakiwa na kuendelea kuongoza kwa muhula wa pili.

**Chanzo: Mtandao**

# GORAN AITAHADHARISHA YANGA UGENINI TABORA

**Na Faustine Feliciane, TABORA**

IKIWA imebaki siku moja kabla ya kuivaa Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Kocha Mkuu wa Tabora United, Goran Kopunovic, amesema mabingwa hao watetezi wasitarajie mteremko katika mchezo huo.

Kwa mara ya kwanza Yanga itashuka kwenye uwanja huo msimu huu baada ya kupita mikoa miaka mingi Tabora kukosa timu ya Ligi Kuu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kopunovic, alisema anaifahamu vizuri Yanga ni miongoni mwa timu kubwa nchini, hivyo amefanyia kazi mbinu zao na anaamini watawapa upinzani mkubwa ili kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu za mchezo huo.

Kopunovic alisema baada ya kupoteza mchezo uliopita dhidi ya Ihefu, ametumia muda mwingi kufanyia kazi mapungufu aliyoyabaini na sasa wapo tayari 'kuwasimamisha' mabingwa hao watetezi.

"Hautakuwa mchezo mwepesi, ni mchezo mgumu kwa kila timu, Yanga wasitarajie mechi nyepesi, tunataka kuvuna pointi tatu jambo hili tumelifanyia kazi muda mrefu," alisema kocha huyo.

Aliongeza Tabora United itakuwa na faida kubwa kucheza na Yanga kwenye uwanja wa nyumbani na mbele ya mashabiki wake.

"Najua mashabiki watakuwa wengi kutokana na ukubwa wa mchezo huu, tutatumia hiyo nafasi kuhakikisha tunapata pointi mbele ya Yanga," Kopunovic aliongeza.

Katika hatua nyingine, uongozi wa Tabora United umeishukuru na kuipongeza Bodi ya Ligi Kuu Nchini na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kuufungulia uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

"Kutumia uwanja wetu ni faida kwa jamii ya Tabora.., kupitia uwanja huu kipindi cha mechi watu wanapata kipato kwa shughuli mbalimbali, Bodi ya Ligi imefanya jambo la maana kufungulia uwanja wetu, tena tunatumia kwenye mchezo mkubwa kama wa Yanga na Simba, watu wengi watafaidika," alisema Pendo.




Wachezaji wa mpira wa kikapu wa Timu ya Vijana wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kwenye viwanja vya JKM Park jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ruvu Shooting 'mwaka wa shetani'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikishika mkia katika Ligi ya Championship, Ruvu Shooting imetolewa kwenye michuano ya Kombe la FA baada ya kufungwa bao 1-0 na Mkwajuni FC ya Songwe inayoshiriki Ligi Daraja la Tatu.

Ikicheza nyumbani kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro Maafande hao walishindwa kupata dawa ya kuwakabili vijana hao wa Songwe na kujikuta waliyaaga mashindano hayo ambayo bingwa hupata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa sasa Ruvu Shooting inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi ya Championship, ikiwa imecheza mechi 14, haijashinda hata mechi moja, ikitoka sare moja na kupoteza michezo 13.

Baada ya kushuka daraja, Ruvu Shooting ilikimbiwa na baadhi ya wachezaji wake ambao wamekimbia kujiunga na timu za Ligi Kuu.

Baadhi ya mechi ambazo imepoteza ni dhidi ya FGA Talents ikifungwa mabao 2-1, ikabamizwa mabao 3-0 dhidi ya KenGold, bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, Copco na Mbeya City, ikachezea kichapo cha magoli 5-0 kutoka kwa Mbuni FC halafu ikafungwa mabao 3-1 na Pamba ya Mwanza.

Ruvu Shooting pia ilikutana na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Biashara United, Stand United na Pan African na kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Transit Camp.

Uongozi wa timu hiyo unatakiwa kukiimarisha kikosi chao katika dirisha dogo la usajili ili kukiongezea nguvu.

# Mapinduzi, African Sports kitaeleweka

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya African Sports na Mapinduzi FC zinaongoza katika msimamo wa First League zamani Ligi Daraja la Pili ambayo inaendelea katika viwanja mbalimbali nchini.

Wakati Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1988, African Sports yenye maskani yake jijini Tanga wakiongoza katika Kundi A, Mapinduzi yenyewe ndio vinara wa Kundi B.

Baada ya mechi za juzi, msimamo wa ligi hiyo unaonyesha African Sports inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 11, imecheza mechi tano, ikishinda mechi tatu, sare mbili, haijapoteza hata mechi moja, ikifunga mabao 10 na kuruhusu matatu.

Malimao FC inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 10, sawa na Nyumbu FC, lakini zinatofautiana idadi ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Dar City ipo katika nafasi ya nne ikiwa na pointi zake tisa, Kiluvya ya Pwani inashika nafasi ya tano ikiwa na pointi nane huku Tunduru FC ikiwa kwenye nafasi ya sita na African Lyon ya Dar es Salaam, zote zikiwa na pointi moja, Lipuli FC ikishika mkia kwa kutokuwa na pointi hata moja.

Mapinduzi FC inaongoza Kundi B ikiwa na pointi 10, ikicheza mechi nne, ikishinda tatu, na sare moja, ikifunga mabao matano na kuruhusu goli moja tu mpaka sasa.

Inafuatiwa na Tanesco FC yenye pointi tisa, ikicheza mechi nne, ikishinda tatu na kupoteza moja, Rhino Rangers ya nne ikiwa na pointi tisa, lakini ikizidiwa uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa na Tanesco FC.

TRA FC iko katika nafasi ya nne na pointi zake saba, Mwadui FC ni ya tano ikiwa na pointi nne, Kurugenzi FC yenye pointi tatu inafuatia huku Alliance FC ni saba ikiwa na pointi mbili wakati Kasulu United inaburuza mkia ikiwa na pointi moja mkononi.

Timu zitakazofanya vizuri katika ligi hiyo inayosimamiwa na TFF zitapanda daraja kucheza Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), katika msimu ujao wa 2024/2025.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ANUKIA JUVE

KLABU ya Juventus inataka kumsajili kiungo wa kati Manchester City na England, Kalvin Phillips, ifikapo Januari, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anaripotiwa yupo tayari kuhama. **(Tuttomercatoweb)**

### PALACE YAMTAKA NKETIAH

KLABU ya Crystal Palace imeonyesha nia ya kumtaka mchezaji wa Arsenal na England, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 24 wakati wa dirisha la uhamisho la Januari. **(Football Transfers)**

### CITY, ARSENAL VITANI

ARSENAL na Manchester City zote zinalenga kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Douglas Luiz, mwenye umri wa miaka 25. **(Football Insider)**

### SANCHO MAMBO MAGUMU

WAWAKILISHI wa winga wa England, Jadon Sancho, wanajaribu kulazimisha uhamisho wa kuondoka Manchester United kwa nyota huyo. Lakini makubaliano ya kubadilishana wachezaji kumhusisha winga huyo mwenye umri wa miaka 23 na Borussia Dortmund huenda yakawa na ugumu. **(Givemesport)**

### ECHEVERRI ANUKIA EPL

CHELSEA na Manchester City zimeomba kufahamishwa kuhusu kiungo wa kati wa River Plate ambaye ni raia wa Argentina, Claudio Echeverri, mwenye umri wa miaka 17**. (Fabrizio Romano)**

### ALABA ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kuwaondoa wachezaji msimu ujao ili kumsajili beki wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, mwenye umri wa 31. **(Fichajes kupitia Football Transfers)**

### EVERTON YAMTAKA NDIAYE

KLABU ya Everton imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji mwenye umri wa miaka 23 wa Marseille na Timu ya Taifa ya Senegal, Iliman Ndiaye. **(Teamtalk)**

### WIEFFER ANUKIA FULHAM

KLABU ya Fulham inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa Feyenoord na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Mats Wieffer, mwenye umri wa miaka 24. **(Football Insider)**

### GUTIERREZ KUTUA MADRID

KLABU ya Manchester City inatarajiwa kuungana na Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kupata sahihi ya nyota wa Girona, Miguel Gutierrez, mwenye umri wa miaka 22, **(Manchester Evening News)**

### HOJBJERG ATAKIWA JUVE

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, mwenye umri wa miaka 28, yuko kwenye orodha ya nyota wanaowindwa na Juventus kwenye dirisha la Januari. **(Tuttosport)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: SIJAFURAHISHWA NA KIWANGO BARCELONA

Kocha huyo aeleza timu yake iliteseka kupata ushindi katika...

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández, alikosoa uchezaji wa timu yake „usiokubalika" licha ya kumaliza mechi tatu mfululizo bila kushinda kwa kuwafunga Almería walio mkiani katika Ligi Kuu Hispania (LaLiga), mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Olimpiki hapo juzi.

Nahodha, Sergi Roberto, alifunga mabao mawili, likiwamo la ushindi la dakika ya 83, na hivyo kuondoka na pointi tatu baada ya Almería kutoka nyuma mara mbili kutafuta ushindi wao wa kwanza kwenye ligi hiyo msimu huu.

„Tuliteseka zaidi kuliko nilivyotarajia," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

„Tulipiga mashuti 30 na kuwapa zawadi ya mabao mawili. Kipindi cha kwanza hakikubaliki. Kama kocha huwezi kukubali hilo... niliwaambia wachezaji hivyo wakati wa mapumziko.

„Ni rahisi kama hivyo. Kipindi cha pili ni bora zaidi, lakini tulikosa nafasi nyingi na tulifanya makosa mengi. Imekuwa hivi kwa zaidi ya mwezi mmoja.

„Timu ilikosa ari. Timu haina ari kama iliyokuwa nayo msimu uliopita. Tunahitaji mdundo na nguvu zaidi."

Raphinha aliipatia Barca bao la kuongoza katika kipindi cha kwanza, lakini Almería ikasawazisha kabla ya kipindi cha mapumziko kupitia kwa Léo Baptistão, jambo ambalo lilipelekea mashabiki wa nyumbani kuwapigia filimbi wachezaji wakati wa mapumziko.

„Ninaelewa kabisa kwa nini walipiga filimbi," aliongeza Xavi. „Sipendi kupigiwa miluzi. Sikuwahi kupigiwa miluzi maishani mwangu, lakini ninaelewa.

„Kama nilivyosema, uchezaji haukubaliki. Unaweza kucheza vizuri, vibaya, kushinda au kushindwa, haijalishi, lakini lazima utoe kila kitu kwa heshima ya klabu."

Roberto alirejesha uongozi wa Barca, Almería ikasawazisha tena, wakati huu kupitia kwa Edgar González.

Lilikuwa bao la 21 ambalo timu hiyo ya Katalunya imeruhusu katika ligi msimu huu, zaidi ya katika kampeni nzima mwaka jana.

Bado kulikuwa na wakati wa kufanya mabadiliko mengine ambapo Roberto alifunga bao ndani ya dakika 10 za mwisho.

Ushindi huo umeifanya Barca kubakia imepitwa pointi sita na vinara wa LaLiga, Girona na nne nyuma ya Real Madrid, ingawa timu zote mbili zina mechi mkononi baadaye wiki hii.

## HABARI MICHEZO



# TEN HAG AWATAKA VARANE, CASEMIRO KUBAKIA UNITED

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag anataka kuwabakisha Raphaël Varane na Casemiro kwenye kikosi cha Manchester United wakati dirisha la uhamisho la Januari linakaribia kufunguliwa, kwa mujibu wa ESPN.

Wachezaji hao wawili wamehusishwa na kuondoka Old Trafford mwezi ujao lakini Ten Hag ameonyesha nia ya kuwabakisha angalau hadi mwisho wa msimu.

Casemiro amekosa kucheza kwa muda wa miezi miwili iliyopita kutokana na jeraha la misuli ya paja, huku Varane akiwa amerejea katika timu hivi karibuni kufuatia kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Huku kukiwa hakuna soka la Ulaya katika kipindi cha mwaka mpya na Ligi Kuu England na Kombe la FA pekee lililobaki kuchezwa, Ten Hag yuko tayari kupunguza ukubwa wa kikosi chake Januari na tayari ameidhinisha uhamisho wa mkopo wa Donny van de Beek kwenda Eintracht Frankfurt.

Jadon Sancho, aliyefukuzwa kikosini tangu Septemba, mwaka huu anatarajiwa kuondoka lakini Casemiro na Varane bado wanachukuliwa ni wachezaji muhimu.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN hali inaweza kubadilika ikiwa wachezaji hao watashinikiza kuondoka, lakini ikitokea hivyo, tayari Ten Hag ataiomba klabu kusajili wachezaji wengine.

Akizungumza katika kongamano la mashabiki juzi, Mkurugenzi wa Michezo wa United, John Murtough, aliwaambia wapenzi wa klabu hiyo watalazimika kuwa na "nidhamu kweli" inapokuja suala la kusajili wachezaji wapya.

"Hatutarajii kushiriki katika dirisha la Januari," alisema Murtough.

"Siku zote kutakuwa na uwezekano wa mikataba karibu na kingo za kikosi, haswa katika kutafuta nafasi kwa wachezaji ambao hawachezi mpira wa miguu kama wanavyotaka.

"Tumeona msimu huu sheria za haki sawa kifedha zina meno ya kweli, hivyo tunapaswa kuwa makini sana ili kuhakikisha tunabaki na kufuata sheria, na tutafanya hivyo.

# Arsenal yakataa kumuuza Nketiah

**LONDON, England**

ARSENAL haitaki kumuuza, Eddie Nketiah, wakati wa dirisha la usajili la Januari, huku mshambuliaji mwenyewe akibainika hataki kuondoka, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye alichezea England kwa mara ya kwanza katika kiwango cha juu Oktoba, mwaka huu anahusishwa na kuhamia katika klabu kadhaa pinzani.

Lakini sasa inaeleweka Arsenal haitazamii kuachana na Nketiah.

Hata kama watalazimika kumuuza basi watataka kiasi kinachoweza kufikia pauni milioni 50 ambazo ni sawa na zile walizomuuza, Folarin Balogun kwenda Monaco msimu wa joto.

Brentford, ambayo imekuwa ikipendekezwa zaidi kutoa ofa huku kukiwa na mustakabali usio na uhakika wa Ivan Toney, bado haijaweka wazi nia yake.

Nketiah amefunga mabao sita na asisti nne katika mechi 23 alizochezea Arsenal msimu huu, ingawa amecheza zaidi ya dakika 60 katika mechi 12 pekee kati ya hizi.

Alimaliza msimu wa 2022/23 akiwa na mabao tisa na asisti tatu katika michezo 39, ingawa tena alitumiwa kwa kiasi na kuelekea mwisho wa michezo kwa sehemu kubwa ya msimu.

Arsenal ilimwongeza Nketiah mkataba utakaodumu hadi mwishoni mwa msimu wa mwaka, 2027.

# Klabu Bundesliga zamgombea Sancho

**MUNICH, Ujerumani**

WINGA wa Manchester United, Jadon Sancho, anawindwa na klabu za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayer Leverkusen, RB Leipzig na Stuttgart, vyanzo vimethibitisha kwa 90min.

Sancho hajaichezea United tangu Agosti, mwaka huu baada ya kutolewa kwenye kikosi cha kwanza kwa kukosana na kocha, Erik ten Hag.

Kocha huyo alipendekeza winga huyo asijumuishwe kwenye kikosi cha siku ya mechi wakati walipofungwa 3-1 na Arsenal kwa sababu ya kiwango duni alichoonyesha mazoezini, lakini Sancho alikanusha hilo katika mitandao ya kijamii na amekataa kumwomba radhi Ten Hag kwa kosa hilo.

Na sasa timu tatu za Leverkusen, Leipzig na Stuttgart zimeonyesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili Sancho.

Mapema mwezi huu, 90min iliripoti Leipzig inakaribia kumpoteza Fabio Carvalho hapo Januari huku Liverpool ikitafuta kukatiza mkataba wake wa mkopo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ambaye amecheza dakika 360 pekee hadi sasa msimu huu.

Kwa hiyo Leipzig wako sokoni kwa chaguo jingine la mshambuliaji na wanamwangaikia Sancho.

Hata hivyo, mshahara wake mkubwa utafanya mpango wowote kuwa mgumu - ikiwa Sancho ataondoka kwa mkopo, United wanataka sehemu nzuri ya mshahara wake kulipwa na wangependelea kujumuisha kifungu cha lazima cha ununuzi.



HABARI MICHEZO

# TWENDE ZETU IVORY COAST KI-VIP, WASHINDI WAZAWADIWA

**Mwandishi Wetu**

WAKATI washindi sita wa Kampeni ya Twende Zetu AFCON Ki-VIP wakitarajiwa kutangazwa Januari 2, mwakani, kampeni hiyo imeendelea kutoa zawadi mbalimbali za siku na wiki, imefahamika.

Fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika AFCON 2023 zitafanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast na washindi sita wanaobashiri na Betika kupitia Tigopesa watakwenda kuishuhudia Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) mubashara kwa gharama za Betika.

Kabla ya droo hiyo kubwa itakayofanyika Januari 2, mwakani, Betika na Tigopesa wamekuwa wakitoa zawadi mbalimbali kwa washindi wanaoendelea kubashiri katika kampeni hiyo.

„Leo (jana) tumekabidhi TV ya nchi 70 kwa mmoja wa washindi wetu wa wiki anaitwa, Emmanuel Anderson," alisema Martin Mavula, Meneja wa Tigo wa Mkoa wa Dodoma.

Awali Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvelinaus, alisema kampeni hiyo inatoa washindi wawili wa televisheni ya nchi 70 kila wiki.

„Hawa wanapata na dikoda yenye kifurushi, vilevile kuna mamilioni ya pesa kwa washindi wa kila siku. Unapoendelea kubashiri nasi kupitia akaunti ya Tigopesa ndipo unajiweka katika nafasi kubwa ya kushinda zawadi mbalimbali na kuingia kwenye droo ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP," alisema.

Mbali na ushindi kwa wateja wa Betika, Rugambwa alisema:"Timu yetu ya Taifa inahitaji sapoti ya Watanzania, Betika kwa kutambua hilo tukaona tutoe fursa hii, lakini ni kwa wale tu wachezaji wetu wanaotumia Tigopesa," alisema.




Meneja wa Tigo Mkoa wa Dodoma, Martin Mavula (kulia), akimkabidhi zawadi ya televisheni mshindi wa Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Emmanuel Anderson (katikati). Kushoto ni Balozi wa Betika Dodoma, Sara Sarakikya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Stars imefuzu kushiriki AFCON kwa mara ya tatu, baada ya kufanya hizo mwaka 1980 huko Nigeria na mwaka 2019 huko Misri.

Balozi wa Betika Dodoma, Sara Sarakikya, alisema ni rahisi kupata nafasi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia mubashara fainali za AFCON.

„Unachotakiwa ni kuweka pesa kwenye Tigopesa yako na kubeti na Betika," alisema na kuongeza.

# Simba yahitaji 9 kufunga mwaka

INATOKA UK. 24

„Nadhani lengo sasa ni kuchukua pointi tisa katika mechi tatu zinazofuata, nilichoona sasa ni vijana wangu wamepunguza ile presha ya mwanzo ya kutopata matokeo, na kwa kweli presha kubwa ilikuwa ni kupata ushindi dhidi ya Wydad, kama tungefungwa, tungepoteza matumaini kabisa na wachezaji wangekuwa katika matatizo.

Lakini baada ya ushindi kila mmoja ana furaha, pia hata sisi makocha inatupa wasaa wa kukaa nao na kuwapa vitu tulivyonavyo na wao wanavichukua kwa utulivu na ukakika," alisema kocha huyo raia wa Algeria ambaye ameichukua timu hiyo kutoka kwa mikono ya Roberto Oliveira ‚Robertinho'.

Aliongeza anaamini mechi hizo tatu za kufungia mwaka ni mgumu, lakini kwa kipindi kifupi tayari amefanikiwa kuwapa mbinu mpya nyota wake na zimesaidia kuwaongezea ubora.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema malengo makubwa ya timu yao ni kuchukua pointi zote katika mechi hizo tatu zilizobakia ili kufunga mwaka.

„Malengo yetu ni kuzichukua alama tisa zote kama zilivyo, ni ngumu, KMC ni wagumu lakini tunakwenda kushinda, tukimalizana na KMC tutakwenda, Kigoma halafu Tabora, kama tumemfunga Wydad, tumecheza mpira mzuri kule Marrakech, tukasumbuliwe kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, au Kigoma, tutashinda japo najua mechi zitakuwa ngumu," Ahmed alisema.

Aliongeza baada ya mechi hizo wataanza maandalizi ya kuelekea katika michuano ya Kombe la Mapinduzi itakayofanyika kuanzia Desemba 28, mwaka huu hadi Januari 13, mwakani huko Zanzibar.

# Simba Queens sasa macho kwa Baobab

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amewapongeza wachezaji wake kwa ushindi mnono wa mabao 5-0 walioupata katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Ceasiaa Queens na sasa waelekeze nguvu katika mchezo unaofuata.

Simba Queens itashuka tena dimbani Jumatano ijayo kuvaana na Baobab Queens kutoka jijini Dodoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema pamoja na ushindi huo, amewataka wachezaji wake wasahau matokeo hayo na kujipanga imara kwa ajili ya mechi inayofuata.

Mgunda alisema licha ya kupata ushindi huo, alikiri wapinzani wao Ceasiaa Queens waliwapa ushindani mkubwa hasa kipindi cha kwanza.

Alisema baada ya kuwasoma kipindi cha kwanza na kuyajaua mapungufu yao na ubora walionao, kipindi cha pili walimudu vizuri na kuondoka na pointi tatu.

„Tumeanza vizuri na ushindi huu ni ishara nzuri kuelekea katika mechi zetu zijazo, ulikuwa ni mchezo wenye ushindani mkubwa, hatukuwajua wapinzani wetu kipindi cha kwanza tukawasoma vizuri na kutumia mapungufu yao kupata ushindi wa mabao 5-0. Hii imepita, sasa tunaangalia mechi zijazo," alisema Mgunda.

Kuhusu straika, Aisha Mnunka, alisema ni mchezaji mzuri, ukiangalia kimo chake unaweza usimpe jezi lakini amefanya vizuri na ninaimani atafanya vizuri zaidi.

"Nina wachezaji wazuri, kina Aisha wengi wapo, nitafanya mabadiliko katika mechi zijazo, tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kujiandaa na mechi ijayo ili kufanya vizuri, ukizingatia ligi ni mbio ndefu na kila timu imejiandaa vyema," alisema kocha huyo.

Mnunka ambaye juzi alifunga hat-trick alisema malengo yake ni kuendelea kufunga kuisaidia timu na hatimaye kuibuka mfungaji bora wa ligi hiyo msimu huu.

# Yanga: Tabora United jipangeni

INATOKA UK. 24

za mwisho na wamejipanga kuendelea kuwapa furaha mashabiki na wanachama wao.

Walter alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali kwa sababu wanahitaji kukusanya pointi na hatimaye kurejea katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo.

„Tumejipanga kwenda kupambana, hakuna mechi rahisi, kila mchezaji wa Yanga anafahamu hilo, hatutabweteka na matokeo ya mechi yetu iliyopita ya CAF, tunawaheshimu wapinzani wetu," meneja huyo alisema.

Yanga itashuka dimbani kesho ikiwa pia na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, mechi yake ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mabingwa hao watetezi wana pointi 27 kibindoni na wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara nyuma ya vinara, Azam FC yenye pointi 28, lakini Yanga wakiwa na michezo miwili mkononi.

Simba yenye pointi 22 lakini imeshuka dimbani mara tisa itacheza mechi yake nyingine ya ligi hiyo yenye kushirikisha timu 16 keshokutwa dhidi ya KMC FC, zote za Dar es Salaam.

Wakati huo huo, Yanga itaanza kuwania Kombe la Mapinduzi kwa kucheza dhidi ya Bandari FC ya Kenya Desemba 31, mwaka huu wakati Januari Mosi, mwakani Simba itawavaa Jamhuri huku Desemba 30, mwaka huu Azam FC itachuana na mabingwa watetezi, Mlandege.

Michezo

Ijumaa Desemba 22, 2023
Nipashe

Xavi: Sijafurahishwa na kiwango Barcelona UKURASA 21



# YANGA: TABORA UNITED JIPANGENI

●●● Itaanza na Bandari ya Kenya katika Kombe la Mapinduzi...




Kipa wa Yanga, Djigui Diarra (kulia), akimpa maelekezo beki wa timu hiyo, Nickson Kibabage, katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

**Na Faustine Feliciane, TABORA**

WAKATI timu bado ikiwa na joto la ushindi wa mechi ya mashindano ya kimataifa, benchi la ufundi la Yanga limesema watatumia nguvu ile ile kuikabili Tabora United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi uliokoo mkoani Tabora.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watawavaa wenyeji Tabora United ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0 walioupata dhidi ya Medeama kutoka Ghana katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema tayari wameshasahau matokeo ya mechi iliyopita ya mashindano ya kimataifa na sasa wanageuza 'silaha' zao kuhakikisha wanaenda kupambana kupata ushindi dhidi ya Tabora United.

Gamondi alisema baada ya kumaliza mechi hiyo, kikosi chake kilirejea kwenye uwanja wa mazoezi na kufanyia kazi mapungufu waliyoyabaini kwa ajili ya kuhakikisha wanaenda Tabora kuchukua pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema kila mchezo una mipango yake na Yanga imejipanga kuingia tofauti katika mechi ya kesho dhidi ya timu hiyo mpya iliyopanda daraja msimu huu.

„Tunaenda kukabiliana na Tabora United kwa mbinu nyingine, tunataka kuendeleza ushindi katika michezo yetu ya Ligi Kuu ingawa nafahamu mchezo hautakuwa mwepesi kutokana na ratiba ya timu yangu," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema wachezaji wake lazima wakapambane na kujituma licha ya uchovu walikuwa nao baada ya kutoka kucheza mchezo mgumu wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

„Nina imani na wachezaji, kwetu kikubwa ni ushindi... tutacheza na Tabora United huku tukiwa na lengo moja tu la kusaka ushindi, tutapambana kufanikisha hili," alisema Gamondi.

Meneja wa timu hiyo, Harrison Walter, alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yako katika hatua

INAENDELEA UK. 23

# Simba yahitaji 9 kufunga mwaka



**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwachapa Waarabu wa Morocco, Wydad mabao 2-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Jumanne iliyopita, kikosi cha Simba kinataka kuvuna pointi tisa za Ligi Kuu Tanzania Bara ili kufungwa mwaka 2023 kwa shangwe.

Simba inatarajia kucheza dhidi ya KMC keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam halafu itaelekea Kigoma kukutana na Mashujaa mechi itakayochezwa Desemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na baadaye kuwafuata Tabora United mkoani, Tabora, mchezo utakaopigwa Desemba 29, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema baada ya kushinda mechi dhidi ya Wydad sasa kila kitu kinakwenda sawa na amekuwa na uwanja mpana wa kuendelea kuwatengeneza wachezaji wake kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi.

Benchikha alisema anahitaji kuona ari ya vijana wake inaimarika zaidi kuelekea mechi hizo tatu muhimu zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema anaamini watashuka dimbani kukutana na KMC, Mashujaa FC na Tabora United huku wachezaji wake wakiwa hawana presha kama ilivyokuwa katika michezo mingine iliyotangulia.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042